Nipashe
Alhamisi Februari 20, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580159
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Kijana afa kwa kugonga treni, akutwa na msokoto wa bangi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Lissu amlipua Mashinji

• **Asema** alikosa uadilifu ndani ya Chadema, adai hakuna pengo kuondoka kwake... *Endelea ukurasa 2*



LISSU MASHINJI

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**MWANAFUNZI AELEZA JINSI ALIVYOBAKWA**
MWANAFUNZI wa kidato cha nne ambaye pia ni shahidi wa kwanza kwenye kesi ya ubakaji, ameeleza...

UKURASA WA 5
**UTAFITI WAIBUA ATHARI MPYA ZA MINYOO**
WATAALAM na watafiti wa magonjwa yanayotokana na minyoo yenye madhara kwa mifugo na binadamu...

UKURASA WA 25
**WALIOFARIKI KWA CORONA WAONGEZEKA**
MAOFISA nchini China wamesema idadi ya watu waliofariki dunia kutokana na ugonjwa wa virusi vya Corona...

## Kicheko kushuka bei ya mbolea

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store



## Mbatia ashtukia kauli za viongozi kuelekea uchaguzi

UKURASA 2

**MICHEZO** HAMSINI ALIA POLISI KUDHULUMIWA BAO UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbatia ashtukia kauli za viongozi kuelekea uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amewataka viongozi na wanasiasa nchini kuchunga ndimi zao na kupima kauli wanazozitoa wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu.

Mbatia ambaye pia ni Mbunge wa Vunjo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akifungua kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho.

Alisema kuelekea uchaguzi mkuu, viongozi na wanasiasa hawana budi kupima kauli na kuchunga ndimi zao ili uchaguzi unafanyike katika hali ya utulivu na amani badala ya kumwaga damu.

"Watanzania ninachowaomba tupunguze majungu, umbea, fitina, kusema uongo, kujenga chuki na umaskini wa kufikiri. Mwaka huu ni wa ni uchaguzi, hivyo tunatakiwa tushiriki katika uchaguzi huo kwa hoja zenye mashiko bila matusi. Tushindane kwa hoja na Watanzania waamue pumba ni ipi na mchele ni upi.

"Twende kwenye hoja za kutushirikisha pamoja na tusitishane. Tutoe lugha chanya zenye kueleweka, zenye kuibeba Afrika na kuhakikisha Tanzania inakuwa kielelezo sahihi na kimbilio la dunia na 'umimi' tuuondoe," alishauri.

Mbatia alisema ni jambo la kushangaza kuona viongozi, hasa wanasiasa, wanakuwa hawaeleweki kutokana na kauli wanazozitoa.

"Mwanasiasa jana unamsikia kasema hiki, leo anasema hivi, kesho anasema vile, anazungumza kauli tata tu. Nawashauri wanasiasa kabla ya kutamka jambo lolote, wamwombe sana Mwenyezi Mungu, kwamba 'kilinde kinywa changu'.

"Unakuta mtu mzima anaongea vitu vya ajabu, ina maana ulimi unateleza kila siku na hata watoto wanakuwa wanakushangaa, na wakiangalia hizo 'clips' kwenye mitandao, wanasena 'huyu ni baba wa namna gani?'.

"Tuliandika kitabu kwamba upinzani siyo uadui, kuwa na mawazo au fikra mbadala siyo uadui, kuna watu wanadhani kuwa chama mbadala ni uadui.

"Dunia ya leo inazungumzia ushirika wa kidunia, haizungumzii ushindani wa kidunia, sasa sisi Tanzania tumekuwa kwenye vyama vya siasa, tunatakiwa kushindana kwa hoja na si kwa matusi wala kwa kejeli, mifarakano au kumwaga damu, badala ya kusema yangu, tuseme yetu," alishauri.

Mbatia pia aliwaomba Watanzania kuacha kushindana na kujenga tabia ya kufanya mazungumzo ya kuridhiana pale wanapoona mambo hayaendi sawa.

Kiongozi huyo wa NCCR-Maguezi pia aliwaalika wanaohama kutoka vyama vyao kwenda Chama Cha Mapinduzi (CCM), kufikiria kwenda kwenye chama chake kikiongeza nguvu.

Mbunge ya Moshi Vijijii, Anthony Komu (Chadema), alisema kuna haja vyama vya upinzani kushughulikia matatizo ya ndani ya vyama ili kupunguza wimbi la wanachama wake kuhama.

"Tunafahamu kwamba mtu kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine siyo dhambi na ni haki yake kikatiba, lakini pia kuna haja ya vyama kukaa na kujitafakari na kushughulikia matatizo ya ndani na si kunyamaza kimya na kupuuzia," alisema.

Komu alisema hana mpango wa kuhamia CCM kama ambavyo amekuwa akitajwa mara kadhaa.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mwita Waitara, akisalimiana na wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wa eneo la Makoroboi, jijini Mwanza jana, wakati alipowatembelea ili kujua namna ya kuwasaidia baada ya kupoteza bidhaa zao katika ajali iliyotokea Februari 12 mwaka huu. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Lissu alimpua Mashinji

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amedai uadilifu wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk.Vicent Mashinji, kwa chama ulikuwa hafifu.

Lisu amedai kuwa hiyo ndiyo sababu iliyousukuma uongozi wa juu wa chama hicho kuchukua uamuzi wa kumwondoa madarakani mapema.

Juzi, Dk. Mashinji alitangaza kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ikiwa ni takriban miezi miwili tangu alipoondolewa katika nafasi ya Katibu Mkuu wa Chadema. Nafasi yake ilichukuliwa na Mbunge wa Kibamba, John Manyika.

Kabla ya uteuzi huo, Mnyika alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Tanzania Bara.

Msomi huyo alidai baada ya kupokewa CCM na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, alidai: "Miaka 47 bado ni kijana, kama Rais Magufuli anavyosisitiza maendeleo hayana chama, hivyo nimwombe Mwenyekiti wa CCM kama ataridhia anikubalie nijiunge na chama hiki.

"Baada ya kutafakari mwenendo mzima wa siasa na uchumi nchini na kuangalia kina nani wako tayari, nikaona kwa upande wetu Chadema bado tuko mbali sana kuchochea mambo haya ya maendeleo."

Wakati Dk. Mashinji akitoa kauli hiyo muda mfupi baada ya kuondoka Chadema, Lissu akizungumza na Nipashe jana, alidai kuondoka kwa kiongozi huyo kunathibitisha kuwa uwezo wake wa kusoma kile alichokiita alama za nyakati ni mdogo.

"Chama chetu kilikuwa sahihi kumwondoa kwenye nafasi hiyo. Uwezo wake wa kusoma alama za nyakati na uadilifu wake kwa chama ulikuwa hafifu," alisema.

Lissu alisema Dk. Mashinji na viongozi wengine waliotangulia kuondoka katika chama hicho kwa siku za karibuni, walichelewa kuchukua uamuzi huo, akifafanua kuwa walipaswa kuondoka wakiwa tayari wana vyeo ndani ya Chadema.

Alidai kuondoka kwao katika kipindi hiki hakuna madhara kwa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

"Yeye pamoja na wenzake waliomtangulia kuondoka siku za karibuni, walichelewa sana kuondoka, walitakiwa waondoke wakiwa bado wana vyeo ndani ya chama, ingetutia doa, wameondoka baada ya chama kuwatema kwenye uongozi, hawana madhara," alisema.

Dk. Mashinji alijiunga na CCM ikiwa ni siku moja baada ya aliyekuwa mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Chadema, Cecil Mwambe, kujiuzulu ubunge wa Ndanda na kuihama Chadema.

Mwishoni mwa mwaka jana, Waziri Mkuu mstaafu, Fredrick Sumaye, alitangaza kujivua uanachama wa Chadema kutokana na kile alichodai kukosekana kwa demokrasia ndani ya chama hicho na baadaye kurejea CCM alikotoka mwaka 2015.

Mwanasiasa mwingine ambaye alirejea CCM baada ya kujiengua mwaka 2015 ni aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa.

Lowassa alijiunga na Chadema baada ya kukatwa katika kinyang'anyiro cha kumtafuta mgombea urais wa CCM. Alipewa nafasi ya kuwania urais baada ya kujiunga na Chadema na kushika nafasi ya pili nyuma ya mgombea wa CCM, Dk. John Magufuli, ambaye aliibuka kidedea.

## HABARI KITAIFA

# Kijana afa kwa kugonga treni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIJANA ambaye hajafahamika makazi yake, anayekadiliwa kuwa na umri wa miaka (25-30), amefariki dunia baada ya kugonga treni iliyokuwa ikitoka Mwanza kwenda Dar es Salaam.

Kijana huyo alikutwa na mauti hayo katika maeneo ya Ibinzamata Mjini Shinyanga jana asubuhi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, tukio hilo limetokea katika reli ya kati kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam.

Kamanda Magiligimba, alisema kuwa baada ya kijana huyo kuigonga treni hiyo, mwili wake ulisambaratishwa vipande kutokana na kukanywagwa na kusababisha kifo chake papo hapo.

"Wakati wa kumsachi kwenye mifuko yake ya suruali ili kupata mawasiliano ya ndugu zake, tulimkuta akiwa na msokoto mmoja wa bangi," alisema Kamanda Magiligimba.

Aidha, alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, kwa ajili ya kutambuliwa na ndugu zake ili wafanye taratibu za maziko.




Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kutangaza bei elekezi ya mbolea ya kukuzia (UREA) msimu wa kilimo 2019/2020. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Moses Mabamba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima kicheko mbolea kushuka bei

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imetangaza kushuka kwa bei ya mbolea ya kukuzia ya Urea na nyinginezo, hatua ambayo itawanufaisha wakulima.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya ya ushindani wa zabuni za ununuzi wa mbolea kwa pamoja (BPS) iliyofunguliwa Juni 21, mwaka jana.

Hasunga alisema bei elekezi katika maghala ya Dar es Salaam kwa mfuko wa kilo 50 itakuwa Sh. 43,104 .

"Bei elekezi ya rejareja kwa mkulima kwa mbolea aina ya Urea kwa mikoa ya Kanda ya Mashariki, Kati, Kusini na Kaskazini zitakuwa kati ya Sh. 44,800 na 53,400 kwa mfuko wa kilo 50 wakati kwa mikoa ya Kanda ya Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa, bei elekezi itakuwa kati ya Sh. 50,000 na 57,300 kwa ujazo huo,"alisema Waziri Hasunga.

Kwa mujibu wa Waziri Hasunga, bei hizo zitaanza kutumika leo.

"Ikumbukwe kwamba hizi ni bei za ukomo wa juu katika ngazi za bei ya ghalani, jumla na ya mkulima katika eneo husika, hivyo wafanyabiashara wanaweza kuuza chini ya bei elekezi bila kuathiri ubora wa mbolea," alisema.

Alisema kwa kuzingatia hilo, wizara imetoa bei elekezi ya jumla na rejareja za mbolea kwa uzani wa kilo 50, 25, 10 na 5 katika kila kituo cha mauzo.

Sambamba na hilo, Waziri alionya kuwa ni kosa kisheria kuuza mbolea kwa bei ya juu ya bei kikomo kwa nia ya kujiongezea kipato.

Waziri alibainisha kuwa iwapo kutakuwa na tofauti ya gharama za usafirishaji katika baadhi ya maeneo ambayo itakuwa haiendani na bei elekezi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wameagizwa kukaa na kamati za pembejeo na kurekebisha bei hizo ili ziendane na hali halisi ya kuwezesha usambazaji na upatikanaji wa mbolea kwa wakulima.

Waziri Hasunga alisema katika msimu wa 2019/20, mahitaji ya mbolea ni tani 586,604. Na hadi jana upatikanaji ulifikia tani 491,659 sawa na asilimia 84.

Alibainisha kuwa kati ya Julai Mosi, mwaka jana na juzi, tani 17,832 za mbolea na visaidizi vya mbolea zilitengenezwa nchini. Alisema kati ya hizo, tani 17,157 zilitengenezwa na kampuni ya Minjingu na kampuni zingine 10.

"Zaidi ya asilimia 90 ya mbolea zinazotumika nchini kwa sasa, huagizwa kutoka nje ya nchi. Hivyo, katika kutengeneza mjengeko wa bei, gharama mbalimbali huzingatiwa. Kwa kuzingatia viwango vya ubadilishaji fedha Januari 10, mwaka huu, ilikuwa Sh. 5,300," alisema ,

Aidha, alisema kushuka mbolea kutasaidia kuongeza uzalishaji ikiwamo kuwapo kwa utoshelevu wa chakula na malighafi za viwanda ili Tanzania ifikie njozi yake ya uchumi wa kati unaotegemea viwanda.

**Waziri Hasunga alisema katika msimu wa 2019/20, mahitaji ya mbolea ni tani 586,604. Na hadi jana upatikanaji ulifikia tani 491,659 sawa na asilimia 84**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA "BIOMETRIC VOTER REGISTRATION" (BVR) KATIKA MIKOA YA DAR ES SALAAM NA PWANI**

**TAREHE 14 - 20/02/2019**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. kuwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia Teknolojia ya Biometric Voter Registration (BVR) litafanyika kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | SIKU: | Tarehe **14/02./2020. hadi tarehe 20/02/2020** Mikoa ya Dar es Salaam naPwani |
| 2. | VITUO: | Zoezi la Uboreshaji litafanyika katika vituo vilivyoko katika Mitaa na Vijiji katika Kata zote za mikoa hiyo |
| 3. | MUDA: | Vituo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni. |

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA UTAHUSISHA MAMBO YAFUATAYO:-**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wote wapya ambao ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria watakaokuwa wametimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na wale watakaotimiza umri wa Miaka 18 siku ya Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2020
2. Mpiga Kura ambaya anayo Kadi ya Mpiga Kura ya zamani na imeharibika, imefutika maandishi au kukosewa taarifa zake anatakiwa kwenda kituoni kwa ajili ya kupatiwa kadi mpya
3. Kuandikisha wale wote ambao wanazo sifa lakini hawakujiandikisha mwaka 2015'
4. Mwananchi ambaye ni mara ya kwanza kuandikishwa,atakapofika Kituoni atachukuliwa alama ya vidole vyote kumi vya mikono yote miwili na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
5. Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni. Watu wenye Ulemavu, Wagonjwa, Wajawazito, Akina Mama wanaonyonyesha na Wazee watapata kipaumbele.
6. Mwananchi anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Uandikishaji wa Kituo.
7. Wapiga kura wa Kata ya Kibuta, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mkoani Pwani waliojiandikisha kwenye zoezi la Majaribio tarehe 29 Machi 2019 hadi tarehe 4 Aprili, 2019 wanatakiwa kwenda vituoni tena ili taarifa zao ziweze kuingizwa rasmi katika Daftari la Kudumu la awapiga kura

215632302

**KUMBUKA:**

- SIFA MUHIMU YA KUKUWEZESHA KUTUMIA HAKI YAKO YA KUCHAGUA KIONGOZI UNAYEMTAKA NI KUJIANDIKISHA KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA
- NI KOSA LA JINAI KUHARIBU KWA MAKUSUDI AU KUUZA KADI YAKO YA KUPIGIA KURA
- TANZANIA YA SASA NA IJAYO IKO MIKONONI MWAKO, NENDA KAJIANDIKISHE ILI UWEZE KUPIGA KURA UCHAGUZI MKUU 2020
- KURA YAKO NI KADI YAKO, NENDA KAJIANDIKISHE.

Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar es Salaam
Tel.+255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.



Wakazi wa Mtaa wa Dome, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, wakiangalia mwili wa marehemu Nkuba Mawe (27), ambaye amedaiwa kufariki dunia kwa kunywa pombe kupita kiasi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Korti yahoji hatua upelelezi kesi ya maofisa wa LHCR

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeuagiza upande wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili maofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHCR),Tito Magoti (26) na Mtaalamu wa Tehama, Theodory Gyan (36), tarehe ijayo kueleza upelelezi umefikia katika hatua gani ili iweze kujua unakwenda mbele ama umesimama.

Tito na mwenzake wanakabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kumiliki programu ya kompyuta iliyotengezwa mahususi kufanya kosa la uhalifu na kutakatisha Sh. milioni 17.3.

Amri hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Janeth Mtega, baada ya upande wa Jamhuri kudai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai upelelezi haujakamilika.

Hata hivyo, upande wa utetezi ulidai Februari 5,mwaka huu upande wa Jamhuri ulieeleza mahakamani kuwa upelelezi upo katika hatua nzuri, na kwamba hiyo ni mara ya tano kesi inatajwa na hoja zinazoelezwa ni hizo hizo.

"Mheshimiwa hakimu tunashindwa kuelewa tunakwenda tunarudi nyuma, tunaomba mahakama yako iamuru Jamhuri upelelezi ukamilike badala ya kwenda mbele na kurudi nyuma,"alieleza Wakili wa utetezi, Jebra Kambole. Alidai kazi ya Mahakama si kuahirisha kesi tu, bali inaweza kutumia mamlaka yake kusimamia uchunguzi kwa kuwa katika kesi hiyo hakuna anayejua upelelezi huo utakamilika lini.

Kambole alieleza kuwa siyo tabia nzuri kwa upande wa mashtaka kubadilisha badilisha maneno, na kwamba washtakiwa mpaka sasa hawana dhamana, wapo ndani na hawajui upelelezi utakamilika lini. "Washtakiwa ni binadamu kama sisi, kinachowatokea wao kitamtokea mtu yeyote mahakamani hapo muda wowote, wana familia, wana ndugu na marafiki wanaohitaji msaada wao" alidai Kambole.

Akijibu hoja za utetezi kuhusu upelelezi, Wankyo alidai kuwa maneno yake yapo wazi kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, na kuwaondoa hofu upande wa utetezi kwamba wawekezaji wanaipenda sana Tanzania na watakuja kuwekeza.

Alisisitiza kuwa wanawahimiza wapelelezi kukamilisha upelelezi ili kuondoa malalamiko hayo. Kesi iliahirishwa mpaka Machi 4, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Mapema mahakamani hapo upande wa Jamhuri uliwasomea mashtaka washtakiwa uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Joseph Pande na Wankyo Simon.

Katika kesi ya msingi, Wankyo alidai washtakiwa wote, katika tarehe tofauti kati ya Februari Mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya Jiji la Dar es Salaam na mahali tofauti nchini kwa pamoja na watu ambao hawapo mahakamani, kwa makusudi walishiriki kutenda makosa ya kiuhalifu ya kumiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kufanya kosa la jinai na kuwawezesha kujipatia Sh. 17,354,535.

Nchimbi alidai katika tarehe tofauti kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya jiji na mkoa wa Dar es Salaam kwa pamoja washtakiwa hao na wengine ambao hawapo mahakamani, walimiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kutenda makosa ya jinai.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK (TZ) LTD** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana(mali) iliyodhamin mkopo huo kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI | MAELEZO DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SAMADY(TANZANIA)LTD | RAJABU RAMADHANI KHATIBU | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja na.11 Kitalu "Y" Hati na.43574 ofisi ya ardhi na.145771 eneo la Magomeni Dar es salaam. | 14/03/2020 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na,**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Equity Bank (Tz)Limited**
**Head Office,**
**Ohio street-Golden Jubilee Towers,**
**P.O. BOX 110183,**
**DAR ES SALAAM**
**Email: info@equitybank.co.ke**

215638102


# Mwanafunzi asimulia alivyobakwa na mshtakiwa hadi kupata ujauzito

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MWANAFUNZI wa kidato cha nne ambaye pia ni shahidi wa kwanza kwenye kesi ya ubakaji inayomkabili Boniface Malila (20), amedai kumtambua mshtakiwa huyo kuwa ndiye aliyempatia ujauzito.

Mshtakiwa huyo, mkazi wa kijiji cha Katemwa, Chato mkoani Geita, anakabiliwa na kesi ya kumbaka na kumsababishia mimba ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha nne (jina lake na shule vinahifadhiwa).

Mbele ya Mahakama ya Wilaya ya Chato, mwanafunzi huyo ambaye aliongozwa na mwendesha mashitaka wa polisi, Mauzi Lyawatwa, alisema jana kuwa anamtambua mshtakiwa (aliyekuwa kizimbani) kwamba ndiye aliyempatia ujauzito baada ya kufanya naye mapenzi kwa nguvu kwenye nyumba ya kulala wageni ya "Double M" iliyoko Katemwa.

Alidai kuwa alishawishiwa na rafiki yake (jina linahifadhiwa) ambaye pia ni mwanafunzi mwenzake kuwa waongozane kwenda Muganza kumsalimia shangazi yake pasipo kujua kama ilikuwa njama ya kumkutanisha na mshtakiwa.

"Nikiwa na rafiki yangu huyo, tulifika Muganza majira ya saa 12:00 jioni kisha akanipeleka moja kwa moja kwenye eneo alilokuwa anafanyia kazi ya kuchoma muziki na kuingiza kwenye CD kwa kutumia kompyuta huyu Boniface. Baada ya muda mfupi akaniomba nimsubirie pale kwa madai atakuja kunichukua baada ya muda mfupi ili twende kwa shangazi yake," alidai. "Bado nikiwa hapo na huyu mshtakiwa, rafiki yangu alikuja na bodaboda muda wa saa 2:00 usiku baadaye akadai kuna kitu amekisahau alikokwenda na kwamba niendelee kumsubiri mpaka atakapolejea. Ilipofika saa 4:00 usiku, Boniface akadai anapafahamu alipo rafiki yangu na kwamba anipeleke kwa kuwa ilikuwa usiku naye amefunga kazi zake," aliendelea kudai.

Shahidi huyo alidai kuwa katika hali isiyo ya kawaida, alijikuta amefikishwa kwenye nyumba ya kulala wageni ya "Double M" chumba namba tatu na alipohoji kulikoni kampeleka eneo hilo, alitishiwa kuondolewa humo na kunyimwa nauli ya kurejea shuleni kwao iwapo hatakubali kufanya mapenzi na mshtakiwa. Kutokana na hali hiyo na akiwa hajahiari, alidai alisukumizwa kitandani na kuanza kuvuliwa nguo za ndani kabla ya kutii azma ya mshtakiwa ambaye walilala pamoja hadi asubuhi licha ya kupatwa na maumivu makali na kutokwa damu sehemu za siri, kutokana na kuwa ni mara yake ya kwanza kufanya mapenzi na mwanamume.

Alidai kuwa baada ya kutendewa ukatili huo kwa siku mbili mfululizo, alionana na rafiki yake siku ya tatu katika ofisi ya mshtakiwa kabla ya kupewa Sh. 6,000 kwa ajili ya nauli ya kurejea kwao.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, alimpatia mshtakiwa fursa ya kumwuliza maswali shahidi.

Mahakama iliamuru mshtakiwa kurudi mahabusu hadi kesho baada ya wadhamini wake kushindwa kukidhi masharti ya dhamana ikiwa ni pamoja na kuweka bondi ya maneno ya thamani ya Sh. milioni 10 kila mmoja.

HABARI KITAIFA

# Utafiti waibua mambo mapya athari za minyoo

**Na AsrajiMvungi,** ARUSHA

WATAALAM na watafiti wa magonjwa yanayotokana na minyoo yenye madhara kwa mifugo na binadamu, wamewasilisha matokeo ya utafiti wa athari za minyoo hiyo uliofanyika katika mikoa ya Arusha na Iringa.

Wakizungumza jana wakati wa kukabidhi utafiti huo, wataalam hao walisema matokeo yanaonyesha kuwa tatizo hilo ni kubwa na licha ya kuathiri mifugo na kuwasababishia wafugaji hasara pia linatishia usalama wa binadamu, hivyo jitihada za kudhibiti zinahitajika.

Ripoti hiyo ilikabidhiwa kwa watendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kushuhudiwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Prof. Hazuruni Longa, alisema utafiti huo unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 50 ya mifugo wakiwamo ng'ombe wameathiriwa na magonjwa ya minyoo.

Prof. Longa alisema kuna athari kubwa kwenye mazao ya mifugo ikiwamo nyama kutokana na maini yanayopimwa kubainika kuwa na magonjwa hayo, hivyo kutokufaa kwa matumizi ya binadamu.

Mmoja wa watafiti na wadau wa mifugo, Mtafiti Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Dk. Jahashi Nzalawale, alisema katika utafiti wao pia waliangalia uwezo wa dawa zinazotumika kukabiliana na minyoo hao na kubaini kuwa kati ya aina tano za dawa zilizokuwa zimethibitishwa, baadhi zimeshaanza kuwa sugu.

Dk. Nzalawahe alisema kwa sasa wakiwa watafiti, hawana mamlaka juu ya changamoto hizo na kwamba wanachofanya ni kulifikisha suala hilo kwenye ngazi husika.

"Hatua hii ya kukutana na watendaji wa wizara ni sehemu ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo," alisema Dk. Nzalawahe.




Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndungile (wa pili kulia), pamoja na wanachama wa Klabu ya Rotary 'E Club ya Masaki' na benki ya DTB, wakikabidhi msaada wa vifaa vya kujifungulia kwa mama anayetarajia kujifungua Janeth Ernest, katika hospitali ya Mbagala Rangi Tatu jijini humo jana. Takribani wakina mama watarajiwa 350 wamepatiwa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 8.5, chini ya udhamini wa Benki hiyo, ili kuwasaidia kujifungua salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri apigia debe utalii Ukerewe

**Na Lusungu Helela,** UKEREWE

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewataka wananchi kuchangamkia fursa za utalii zilizoko katika Kisiwa cha Ukerewe

Akizungumza jana alipotembelea Kituo cha Urithi wa Utamaduni cha Mapango ya Handebezya kilichoko katika kisiwa hicho mkoani Mwanza, Kanyasu alisema kisiwa hicho ni Zanzibar ya Tanzania Bara

Kanyasu alisema ndani ya kisiwa hicho kuna utajiri wa vivutio vya utalii na hakina tofauti na Zanzibar kutokana upekee wake. Alisema pamoja na vivutio hivyo, kisiwa hicho hakijatumika hicho ipasavyo kama ilivyo Zanzibar.

Kutokana na kauli hiyo, Kanyasu aliitaka jamii kukitumia kisiwa hicho kama fursa ya utalii ili wananchi wafaidike kupitia sekta ya utalii kama ilivyo kwa visiwa vya Zanzibar.

Alisema mbali na Ukerewe kuwa na fukwe nyingi ambazo ni nzuri, pia ina utamaduni wa kipekee ambao ni moja ya mazao ya utalii wenye mvuto wa kipekee unaowafanya watalii wengi kutoka nje ya nchi kujionea amali hizo.

Licha ya vivutio hivyo, Kanyasu alisema katika kisiwa hicho kuna jiwe linalocheza pamoja na jumba lenye ghorofa moja ambalo ni la kwanza kujengwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Kumekuwa na dhana iliyojengeka kuwa watalii wanaokuja nchini wanapenda kutembelea maeneo yenye majumba yenye maghorofa marefu jambo ambalo si kweli bali wanatembelea maeneo ya kawaida lakini yaliyoandaliwa," alisema.

Kanyasu alisema Ukerewe ni hazina katika sekta ya utalii ambayo haijaguswa tokea dunia ilipoumbwa zikiwamo fukwe nzuri, mazingira mazuri na utamaduni wa watu wake

Alisema ngoma pekee yake inaweza kumsafirisha mtalii kutoka Marekani kufika Ukerewe kwa ajili ya kuiangalia kwa sababu ina kionjo ambacho hakiwezi kupatikana mahali popote duniani.

Naibu Waziri alifafanua kuwa utalii wa utamaduni una ladha isiyoisha kwa vile inahusisha viungo vya mwili kucheza tofauti kabisa na mwingine atakavyocheza ngoma hiyo hiyo.

Alisema mbali na utamaduni huo wa kipekee katika kisiwa hicho, pia kuna wanyamapori kama vile mamba na viboko ambao hawajulikani watalii kama wapo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**UZINDUZI WA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UTOAJI WA LESENI ZA UDALALI NA UENDESHAJI WA MINADA YA HADHARA**

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa utoaji wa Leseni za Udalali na Uendeshaji wa Minada ya Hadhara. Mfumo huo utaanza kutumika rasmi kuanzia Jumatatu tarehe 24 Februari, 2020. Hivyo, maombi yote ya Leseni hizo yawasilishwe kupitia Mfumo huo unaopatikana kupitia tovuti ya Wizara (gamisportal.mof.go.tz).

Madalali, Waendesha Minada ya Hadhara pamoja na Wadau wote muhimu mnaombwa kuhudhuria katika uzinduzi wa utoaji wa Leseni kupitia Mfumo huo utakaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Fedha na Mipango – Dar-Es-Salaam siku ya Jumatatu tarehe 24 Februari, 2020 kuanzia saa nne kamili asubuhi. Aidha, Mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo huo yatatolewa siku ya uzinduzi.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu namba +255719520208 na +255713244206.**

**WOTE MNAKARIBISHWA**

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madimbwi mitaani ni hatari msimu wa mvua

**MAMLAKA** ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa utabiri wa mvua za masika ambazo zinatarajiwa kwenye mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka, ikiwamo Dar es Salaam na ukanda mzima wa pwani.

Kwa mujibu wa maelezo ya TMA mvua kubwa na ya juu ya wastani inatarajiwa kunyesha Dar es Salaam na itaambatana na athari mbalimbali.

Utabiri unazielezea sehemu mbalimbali za Dar es Salaam, Zanzibar, Pwani na kanda ya ziwa kuwa zitapata mvua za wastani mpaka juu ya wastani ambazo ni mvua kubwa kwa maeneo mengi.

Wakati angalizo hilo linatolewa ni vyema wananchi wa maeneo hayo wakafuatilia kwa karibu taarifa za hali ya hewa pamoja na kuchukua tahadhari kuepesha madhara ya mvua hizo yakiwamo vifo vinavyotokana na watu kuzama kwenye mito, mabonde na madimbwini.

Pamoja na wanaoishi mabondeni kuhimizwa kuchukua tahadhari ni vyema pia wanaokaa mitaani kwenye mabwawa hasa yaliyotokana na kuchimba mchanga kujiepusha na kuwakinga watoto na hatari ya kuzama majini na kupoteza maisha.

Imekuwa mazoea watu wengi hasa watoto kupoteza maisha kwa kutumbukia kwenye madimbwi yaliyoko mitaani ambayo yalitokana na wafanyabiashara kuchimba michanga bila kujali hatima ya mazingira.

Hili ni tatizo ambalo pengine wakati umefika kwa serikali kuwachukulia hatua wanaosababisha madimbwi kwenye makazi ya watu na hata kuziwezesha mamlaka za maji kuziba au kuendeleza madimbwi au mabwawa hayo ili wavune maji safi badala ya kuyaacha yalivyo.

Wahusika au wafanyabiashara wamekuwa na mazoea ya kuchimba mchanga na kuacha mashimo na makorongo makubwa ambayo mvua zinaponyesha hugeuka kuwa maeneo ya maafa makubwa yanayotishia maisha ya watu.

Pamoja na kuwa chanzo cha mbu na kuongeza tatizo la malaria mitaani, ni mazalia ya wadudu wengine wanaoambukiza magonjwa hasa konokono wa kichocho na mbu wanaoleta dengue.

Lakini, tunachotaka kuwakumbusha wana jamii ni kwamba mabwawa hayo yamekuwa vitanzi vya watoto wa shule, wapita njia, wageni lakini pia mifugo hasa wanyama wadogo kama mbuzi na mbwa.

Aidha, imekuwa ikitumiwa na wahalifu kuua na kutumbukiza watu. Ndiyo maana tunasema kuwa ni vyema kuchukua tahadhari na kuweka uzio kuzunguka mabwawa hayo hasa wakati huu wa mvua. Kadhalika tunawashauri wale wanaokaa karibu na sehemu hizo kuwa makini kwani mabwawa hayo yanapojaa huharibu nyumba na miundombinu ya barabara na mashamba yaliyo jirani hasa baada ya kujaa maji kupindukia na kufurika kwenye kipindi hiki cha mvua.


Tunawashauri wazazi kukumbuka kuwa mvua hizi zitasaidia kuongezeka kwa kina cha maji kwenye mabwawa na mito na pia upatikanaji wa samaki kwenye madimbwi na mabwawa hayo. Tunawakumbusha kuwa wawe makini kwa vile kujaa kwa samaki hao, hasa kambale kunawavutia watoto wanaojitumbukiza mtoni kwenda kuvua. Hivyo bila uangalizi wa karibu wa walezi na wazazi kuna hatari ya watoto kupoteza maisha kwa vile wanapotumbukia mabwawani hawawezi kuogelea wala kuokoa maisha yao.

Ni vyema pia shule zilizo karibu na mabwawa hayo zikawahamasisha wanafunzi kuwa walinzi wa kila mmoja ili kuwaepusha na hatari za kuzama kwenye mabwawa hayo.

Lakini pia, ni wazi kuwa sehemu nyingi watu wanatumia visima vilivyochimbwa. Ni vizuri viongozi wa serikali za mitaa na vitongoji wakashirikiana na wanajamii kuviwekea alama visima hivyo, ili kuepusha uwezekano wa watu kutumbukia hasa wakati huu wa mvua za masika.

Tahadhari hii ni muhimu ili kuwalinda watoto ambao hawawezi kujitetea au wanajamii wengine ambao si wageni wa maeneo hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima



# Kifafa kinatibika, kinaepukwa wanajamii tusimame katika hilo

Na Sabato Kasika

**KIFAFA** ni miongoni mwa magonjwa yanayochanganya jamii hadi kufikia kuamini kwamba kuna uchawi au ni tatizo linaloleta usugu wa akili, hasa katika msongo wa mawazo.

Imani hiyo inadaiwa kusababisha kuendelea kuwapo ugonjwa huo, wakati ukweli ni kwamba baadhi ya watu hawaendi hospitali kupata tiba sahihi, wanaegemea kwa waganga wa kienyeji.

Kwa imani hiyo, baadhi ya watu huwatenga watoto wenye ugonjwa huo wasicheze na wenzao na katika hali hiyo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anaitaka jamii kuondokana na mawazo hayo, anaasa kuwahishwa hospitali wagonjwa wenye kifafa, wapate tiba ya mapema. Inatajwa, wengi hawana ajira nchini na wanakosa wenzi wa kufunga nao ndoa, kutokana na kigezo hicho Waziri Ummy anaisistiza, jamii iondokane na mawazo hayo kwa kuwawahisha wanaoumwa kifafa wapate tiba ya mapema.

Kuna takwimu za kitafiti zinazoeleza asilimia kubwa 36 ya Watanzania, wanaamini kifafa ni ugonjwa unaotokana na uchawi, huku nusu yao wakiamini tatizo linaloleta usugu wa akili, hasa katika msongo wa mawazo.

Ikumbukwe, serikali inagharimu matibabu ya ugonjwa huo katika vituo mbalimbali vya kutoa huduma nchini, hivyo jamii inatakiwa kuhakikisha kila mgonjwa wa kifafa anapelekwa kupata tiba. Imani ambazo ni kinyume zisipewe nafasi, kwani zinachangia kuendelea kuwapo kwa ugonjwa huo, hivyo jambo la msingi ni kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya, ambao kimsingi yako wazi. Ninasema hivyo, kwani wanaeleza wazi kuwa ni miongoni mwa maradhi yanayokabili watu wa rika zote, bila ya kujali jinsia au hali ya maisha na idadi ya wagonjwa wake inakadiriwa kufikia milioni moja.

Aidha, wenye kifafa wako kwenye hatari ya kifo mara sita zaidi, ikilinganisha na jamii yote kwa ujumla na wagonjwa wengi ni vijana.

Hii ni kwa mujibu wa madaktari bingwa wa tiba ya ubongo na mishipa ya fahamu, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, katika mafunzo weliotoa kwa umma jijini Dar es Salaam mwazoni mwa mwezi huu, viwanja wa Bakhera, Manzese jijini Dar es Salaam, maadhimisho ya Siku ya Kifafa Duniani, ambayo kila Jumatatu ya pili ya Februari.

Dk. Petience Njenje anasema kifafa kinatokana na hitilafu au jeraha kwenye ubongo, linalosababishwa na mgonjwa kuanguka akionyesha dalili za kukakamaa kuzimia au kutokuzimia na wakati mwingine anatoa povu mdomoni.

Sababu nyingine za kuwapo kwa kifafa zinaelezwa kuwa ni homa kali kipindi cha utoto, ajali zinazosababisha majeraha katika ubongo, matatizo ya kipindi cha ujauzito na wakati wa kujifungua na minyoo sugu.

Hivyo madaktari wanashauri kujikinga na visababishi vinavyozuilika ikiwamo kuwasaidia wajawazito kwa kuwashauri kwenda kliniki na kupata vipimo mara kwa mara, kufanya uchunguzi, na watoto kutibiwa wanapopata homa.

Suala la matumizi ya choo, kunawa mikono na kula nyama ya nguruwe iliyoiva vizuri ni jambo la muhimu kwa ajili ya kuepuka ugonjwa huo unaotajwa kuwa hatari kwa vijana.

Katika tatizo hili, habari njema ni kwamba, kifafa kinatibika iwapo mgonjwa atapelekwa hospitali mapema kwa ajili ya kupata matibabu, na kwamba atapewa dawa kwa kipindi kirefu bila kuacha.

Lakini bahati mbaya ni kwamba zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa kifafa nchini, wanadaiwa kwenda kutafuta tiba kwa waganga wa kienyeji badala ya kwenda hospitali kupata tiba inayotakiwa.

Inaelezwa na madaktari hao kuwa, asilimia 60 ya wagonjwa wanaofika hospitali kutibiwa, hufika mwaka mmoja baada ya kupata tatizo, huku asilimia tano hadi 10 ya watu wenye kifafa ndiyo hutibiwa hospitalini.

Katika hilo, wengi wanaoishi na ugonjwa huo wakiwa na kifafa cha kiwango cha juu, hali ambayo inatakiwa kuchukuliwa hatua ili kuwasaidia wenye ugonjwa kupata tiba sahihi na hatimaye kupona.

## Diwani aomba kituo cha polisi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

DIWANI wa kata ya Bulamata wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Nicas Nibengo, ameliomba Jeshi la polisi wilayani humo kuanzisha kituo cha polisi katika kata hiyo, ili kukabiliana na matukio ya wizi yanayotokea kwenye kata hiyo.

Ombi hilo lilitolewa hivi karibuni baada ya kusoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kikao cha pili cha Baraza la Madiwani kilichofanyika hivi karibuni wilayani humo.

Nibengo alisema kutokana na kata hiyo kukua haraka kiuchumi kumekuwa na uhalifu wa wananchi kuibiwa mali zao na kukosa msaada kwakuwa kituo cha polisi kuwa mbali na kata hiyo.

"Jambo la msingi tunaomba sana tupate kituo cha polisi kwakuwa Kata ya Bulamata ni kata inayokuwa kwa kasi sana kiuchumi na kituo cha polisi kilichopo kipo mbali kama kilometa 60 kutoka Bulamata," alisema diwani huyo.

Akijibu ombi hilo mkuu wa Jeshi la Polisi wilayani humo, Amon Mimata, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kueleza kuwa kusema tayari suala hilo linafanyiwa kazi ili kuweza kuanzisha kituo hicho.

"Ni kweli changamoto hiyo ipo na nimekuwa nikiwasiliana nae mara kwa mara kuhusiana na matukio madogo madogo ya uhalifu na kwasasa teyari mchakato wa kupeleka kituo hicho umeishaanza," alisema Mimata.

Mbunge wa Mpanda Vijijini, Selemani Kakoso, aliwataka madiwani walioshiriki kikao hicho kushirikisha wananchi katika kuanzisha vituo hivyo kama wanavyofanya kwenye miradi mingine na baadae serikali kumalizia walipoishia.

# Afa akidaiwa kunywa pombe kwa kupitiliza

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NKUBA Mawe (27), mkazi wa Ukenyenge wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, amekutwa amefariki dunia kwenye vibaraza vya maduka ya Mtaa wa Dome, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, akidaiwa kunywa pombe kupita kiasi.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana, ikidaiwa kuwa wananchi wa eneo hilo walibaini kifo cha kijana huyo katika eneo hilo alilokuwa anaishi majira ya saa 12 asubuhi. Ilidaiwa kuwa baada ya kuamka, wakazi wa eneo hilo waliona mtu akiwa amelala kwenye kibaraza cha moja ya duka ya mtaa huo akionekana kama amekufa na waliposogea ndipo wakabaini ukweli wa fikra zao na kutoa taarifa kwa uongozi wa mtaa huo.

Akisimulia tukio hilo Mwenyekiti wa Mtaa wa Dome, Solomoni Najulwa, alidai mara tu baada ya kupewa taarifa na wananchi, alifika eneo la tukio na kubaini kijana huyo alikuwa amefariki dunia na akatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ambalo askari wake walifika na daktari wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa kufanya uchunguzi na kubaini pombe ndiyo chanzo cha kifo hicho.

"Taarifa za awali juu ya kifo cha kijana huyo zilidai aliuawa kwa kupigwa, lakini baada ya daktari kufanya uchanguzi, ilibainika amefariki dunia kutokana na kunywa pombe kupita kiasi," alidai.

Daktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Richard Mwikambe, akiwa eneo la tukio, alisema kijana huyo hajauawa kwa kupigwa, bali amefariki dunia kutokana na kunywa pombe kupita kiasi na akatoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kunywa pombe kwa wingi kwa kuwa ni hatari kiafya.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kueleza kuwa hakuna mtu anayeshikiliwa na jeshi hilo kuhusiana na kifo hicho.

Alidai mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa hadi pale ndugu zake watakapokabidhiwa kwa ajili ya mazishi.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa upanuzi wa barabara ya Bagamoyo kuanzia Mwenge hadi Morocco, katika eneo la Sayansi Kijitonyama, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Watakaokwamisha vita dhidi ya malaria kukiona

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga, ametoa onyo kali na kuahidi kuwachukulia hatua watu watakaobainika kuzuia zoezi la ufukizaji dawa ya mvuke ya kuua mazalia ya mbu na wadudu wadhulifu katika makazi ya watu.

Maganga ametoa onyo hilo wakati wa uzinduzi wa mkakati wa kudhibiti mbu wapevu na wadudu wadhulifu, na kusema kuwa kuna watu ambao wanazusha taarifa za uongo dhidi ya dawa na viuatilifu mbalimbali vya malaria kuwa vina madhara kwa afya ya binadamu.

'Mvuke unaopulizwa hauna madhara, tukigundua kama wewe unataka kukwamisha zoezi hili ili malaria iendelee kututesa tutacheza na wewe mchezo unaoujua wewe na mkuu wa wilaya hili ulibebe," Maganga alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Samson Anga.

Aidha, Maganga alieleza kuwa jamii inapaswa kutambua kuwa kuruhusu uwapo wa malaria kunasababisha madhara makubwa yakiwamo ya kiuchumi, kutokana na kutumia fedha katika matibabu pamoja na kusababisha watu kupoteza maisha.

Ofisa Afya mkoa wa Kigoma, Ambakisye Muhicha, alisema kufuatia uwapo wa dawa za kutosha za kutibu malaria kama Aluu na Mseto, idadi ya vifo vinavyosababishwa na malaria vimepungua kutoka 472 mwaka 2017 hadi vifo 166 kwa mwaka 2019.

Pia alisema kwa 2018 wagonjwa waliobainika kuwa na malaria ni asilimia 28.9 na mwaka 2019 kiwango hicho kilipungua hadi kufikia asilimia 26.7, huku kiwango cha maambukizi ya malaria kwa wajawazito kikishuka kutoka asilimia 11.9 kwa mwaka 2018 hadi asilimia 11.6 kwa mwaka 2019.

Mhicha alisema mafanikio hayo yanatokana na utolewaji elimu ya namna ya kupambana na ugonjwa huo pamoja na upuliziaji wa viuatilifu vya mbu na wadudu katika makazi ya watu ikiwemo dawa ya Ukoko.

Meya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Hussen Luhava, aliwaomba wananchi kuhakikisha wanazingatia maelekezo yatolewayo na watalamu, yanayolenga kuboresha afya zao na kukabiliana na malaria ili kusaidia vita dhidi ya ugonjwa huo

Mkazi wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Khadija Shabani, alisema hafahamu kama kuna dawa za kufukiza za kuua malaria, hivyo ombi lake kwa wanaohusika na masuala ya afya wahakikishe wanaongeza elimu itakayosaidia wananchi kuwa na uelewa, na utakao ondoa ukinzani wa kukataa zoezi hilo

# Maonyesho makubwa ya madini yaja

**Na Joseph Mwendapole**

WIZARA ya Madini imeandaa maonyesho makubwa ya madini yanayotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki hii jijini Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Stanslaus Nyongo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Nyongo alisema kwenye maonyesho hayo wananchi watapata fursa ya kuona aina mbalimbali ya madini na kupata elimu kuhusu yanavyoongezewa thamani.

Alisema maonyesho hayo yataenda sambamba na mkutano wa uwekezaji kwenye sekta ya madini unaotarajiwa kufanyika kesho na keshokutwa katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Julius Nyerere.

Naibu Waziri alisema mkutano huo ni mwendelezo wa mikutano ambayo imewahi kufanyika ambayo Wizara imejiwekea siku maalum za kuongeza na wadau kuhusu changamoto kwenye sekta ya madini.

Alisema kwenye mkutano huo watazindua utoaji wa hati za uhalisia wa madini ya bati yanayozalishwa hapa nchini kama ambavyo utaratibu huo umewekwa na nchi za maziwa makuu.

Naibu Waziri alisema viongozi wa mataifa hayo waliazimia kuanzisha ushirikiano katika kutatua kero zinazosababisha kuwepo kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi zao.

"Viongozi walikubaliana jumla ya maeneo kumi ya kushirikiana ambayo waliyatengenezea itifaki ya pamoja ambayo suala la madini ni itifaki ya tano ambayo inahudu udhibiti wa uvunaji haramu wa madini," alisema Nyongo.

Alisema lengo lilikuwa kuhakikisha madini yanayozalishwa kwenye nchi hizo yanatumika kunufaisha wananchi wake na hayatumiki kuchochea vita kwa wananchi wake kama ambavyo tafiti mbalimbali zilivyoonyesha.

Nyongo alisema ili kuwa na udhibiti wa pamoja nchi hizo zilikubaliana udhibiti uwe kwenye madini ambayo yalionekana kuhusishwa na vita ambayo pia yanapatikana kwenye nchi hizo.

Aliyataja madini hayo kuwa ni bati, tantalum, walframite, dhahabu na kwamba kwa sasa udhibiti umeanza kwenye madini hayo kwa upande wa Tanzania ambapo yanachimbwa kwenye Wilaya ya Ngara na Kyerwa mkoani Kagera.

Aidha, alisema Tanzania inakuwa nchi ya nne kutimiza vigezo ili kuweza kutoa hati za uhalisia kwa madini hayo wakati yanapouzwa nje ya nchi baada ya Congo DRC, Rwanda na Burundi.

Naibu Waziri alisema nchi za Uganda, Jamhuri ya Afrika ya kati na Zambia ziko kwenye hatua za mwisho kukamilisha mchakato huo ili nazo ziruhusiwe.




Vijana waliovalia viatu vya magurudumu, wakiwa wamedandia bajaji iliyoko kwenye mwendo katika Barabara ya Kawawa, eneo la Magomeni Morroco, jijini Dar es Salaam hivi karibuni kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: JOHN BADI**

# Mbunge aonya kuhusu uuzaji ovyo vyakula

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Viti Maalumu (CCM) Mkoani Shinyanga, Azza Hilal, amewatahadharisha wakulima mkoani hapa kuuza vyakula ovyo, ili kukabiliana na baa la njaa.

Hilal alitoa onyo hilo juzi wakati akitoa salamu kwenye mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga, ambao ulikuwa na lengo la kusoma taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Alisema mwaka huu umekuwa na neema ya mvua za kutosha pamoja na wakulima kulima chakula kwa wingi, hivyo ni vyema pale watakapovuna watunze vyakula hivyo kwa akiba ya baadaye na kuacha kuvitumia kwa matumizi ambayo si ya lazima pamoja na kuviuza ovyo.

"Ndugu wajumbe wa mkutano huu, naomba tushirikiane kwenda kutoa elimu kwa wakulima juu ya kutunza vyakula kwa ajili ya akiba ya baadaye kwa sababu mwaka huu mvua zimenyesha za kutosha na wakulima wamelima sana. Ni vyema vyakula hivyo vikatunzwa na huwezi kujua mwakani huenda mvua zikagoma," alisema Hilal.

"Nazungumza haya kwa sababu najua matatizo ya wakulima wetu. Wakiwa na vyakula huwa wanajisahau na kuviuza ovyo wakisema na mwakani tutalima tu. Kinababa huwa wanauza huko huko shambani na kinamama nao wakienda kuchota maji wanaweka kwenye vindoo na kuuza vyakula. Ni bora tuchukue hatua mapema," aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Shinyanga, Edward Ngelela, alikazia suala hilo na kufafanua kuwa kipindi cha kilimo familia huwa zina upendo lakini kipindi cha mavuno huwa kuna ugomvi kutokana na wanaume kuuza vyakula ovyo na kutumia fedha kwa mambo ya anasa.

# Red Cross yaomba ushirikiano Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Busungu John, amewataka wanachama wake Mkoa wa Kaskazini Pemba, kushirikiana katika kukijenga chama chao ili kupiga hatua za maendeleo.

Alisema ushirikiano ndio utakaokiwezesha chama hicho kufanikiwa katika kutekeleza majukumu yake.

Busungu aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, baada ya kufanya ziara ya siku mbili ya kutembelea matawi na kuonana wanachama.

Aliwataka wanachama hao kujitahidi kuongeza wanachama katika chama pamoja na kujituma na kufanya kazi kwa kujitolea.

Aliwaeleza kuwa kwa sasa chama chao kiko vizuri, kwani viongozi ambao wamechaguliwa kukiongoza wamekuwa wakishirikiana katika kukijenga chama hicho bila kuwa na tofauti.

Pia aliwataka wanachama kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kujiletea maendeleo yao na chama chao kwa ujumla.

'Jukumu ambalo nimekabidhiwa na chama chetu ni kuwa mlezi wa Pemba, hivyo ninaloomba kwenu ni ushirikiano na ninawaahidi kusaidia miradi yote ya maendeleo, ambayo mtaianzisha nyinyi kwa ajili ya kukiletea maendeleo chama pamoja na nyie wenyewe," alisema Busungu.

Mratibu wa chama hicho Pemba, Suleiman Ali Mohammed, aliwataka wanachama hao kulipa ada zao kwa wakati.

Katika risala yao, wanachama walimpongeza Busungu kwa kuchaguliwa kwake kuwa mlezi wa chama hicho kwa upande wa Pemba, na kumhakikishia watakuwa na yeye bega kwa bega katika kutimiza wajibu wake.

Walimuomba kuwapatia usafiri pamoja na vitendea kazi ili kutoa huduma kwa jamii na kwa ufanisi.

Katika ziara yake hiyo ambayo ilikuwa ni ya siku mbili, Busungu alitembelea matawi mbalimbali, kufungua tawi jipya la Msuka pamoja na kusaidia vikundi vya ujasiriamali ambavyo vimeanzishwa na wanachama hao.

# Ikungi yabuni mbinu kuongeza makusanyo

**Na Elisante John,** IKUNGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, imebuni utaratibu wa kuwazawadia watendaji wa kata, wanaofanya vizuri na kuongoza kwa kushika nafasi tatu za juu kwenye makusanyo ya mapato ya ndani, yanayotokana na ushuru.

Akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi, alisema utaratibu huo utachangia kuongeza bidii na kuboresha makusanyo ya ndani.

Watendaji walioshika nafasi tatu za juu na kupatiwa fedha kila mmoja kiasi kwenye mabano ni Salida Shinu (250,000) wa Kata ya Iglansoni; Abubakari Maganga (200,000) wa Kata ya Iyumbu na Joseph Mmewa (150,000).

Alisema kupitia njia hiyo anaamini watendaji wa kata wataongeza bidii ya makusanyo kutokana na udhibiti na kubuni vyanzo vipya vya mapato, ambayo yatasaidia pato la ndani kuongezeka, hivyo kukidhi mahitaji halisi ya miradi, itakayotekelezwa na halmashauri ya wilaya.

"Niwahakikishie tu, fedha zote tulizopokea kutoka Serikali Kuu na hizi za makusanyo yetu ya ndani, tutahakikisha zinatumika kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu...kwa utaratibu huu wa zawadi itaongeza motisha na makusanyo ya halmashauri yetu," alisema Kijazi.

Naye, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ali Mwanga, aliwapongeza watendaji waliofanikiwa kupata ushindi, na akawataka waongeze bidii zaidi ili wawe chachu ya kuleta ushindani, dhidi ya wale ambao hawajafanikiwa kufikia malengo ya makusanyo ya ndani.

Aidha, alimpongeza Mkurugenzi na timu yake ya wataalamu kwa kuendelea kusimamia vyema fedha zinazoletwa na Serikali Kuu katika wilaya hiyo kwa ajili ya miradi mikubwa ya maendeleo kama elimu, afya na maji.

# Watumishi, ofisa CRDB kortini tuhuma wizi fedha

**Na Daniel Limbe,** CHATO

JESHI la polisi wilayani Chato mkoani Geita limewafikisha mahakamani vigogo watatu wa serikali pamoja na Ofisa mikopo wa benki ya CRDB kwa makosa ya kughushi nyaraka na kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

Makosa mengine ni kula njama kwa nia ya kutenda kosa pamoja na kuapa kiapo cha uongo kinyume cha sheria za nchi.

Waliopandishwa mahakamani ni Bathromeo Mwikila, Omary Namjombe na Herry Athanas, wote wakiwa ni maofisa wa idara ya elimu kwenye Halmashauri ya wilaya hiyo, pamoja na Leonard Gatawa,mbaye ni ofisa mikopo wa benki ya CRDB Chato.

Mwendesha mashitaka wa serikali, Erasto Anosisye, alidai kuwa washitakiwa hao kwa nia ovu walitumia nafasi zao kutenda makosa kwa nyakati tofauti wakiwa na lengo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume cha sheria.

Kwamba washtakiwa wanakabiliwa na makosa 13 ambayo waliyatenda kwa nyakati tofauti kinyume cha kifungu cha 333,335(d)(i) na 337 cha Sheria ya Makosa ya Jinai sura ya 16 iliyofanyiwa malejeo mwaka 2012.

Aidha, mshtakiwa wa kwanza Bathromeo Mwikila(Ofisa elimu sekondari)na Omary Namjombe, (Ofisa elimu maalumu) wanadaiwa kutumia nyaraka za uongo na kujipatia kiasi cha shilingi 1,727,820 kutoka namba 0152438809000 ya Emanuel Njiku, ambaye ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Buzirayombo pasipo ridhaa yake.

Alidai Novemba 8, 2019 wakidaiwa kughushi kitambulisho cha mfanya kazi pamoja na kutengeneza nyaraka za uongo kwa lengo la kujipatia fedha zikionyesha kuwa Mwalimu Njiku, anahitaji mkopo wa Sh.16,000,000 kutoka benki ya CRDB, wakati wakijua siyo kweli.

Aidha mshtakiwa wa kwanza pekee,(Mwikila), anadaiwa kuwasilisha nyaraka za uongo kwenye Benki ya CRDB tawi la Katoro wilayani Geita, akiwa na lengo la kupewa mkopo akitumia vielelezo vya mwalimu Njiku kinyume cha sheria. Sambamba na hilo, washitakiwa hao pamoja na Ofisa mikopo wa benki ya CRDB tawi la Chato,(Gatawa) wamedaiwa kughushi nyaraka mbalimbali kwa lengo la kuidanganya benki ya CRDB na kujipatia fedha kinyume cha taratibu.

Hata hivyo, baada ya washitakiwa wote kusomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya wilaya hiyo, Odira Amworo, walikana, huku mwendesha mashitaka wa serikali akiiambia mahakama kuwa upelelezi haujakamilika, na kwamba kwa kuwa washtakiwa watatu ni waajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato na mmoja ni mfanyakazi wa CRDB, wote bado wapo kazini wasipewe dhamana ili kupisha uchunguzi zaidi.

Baada ya maombi ya upande wa mashtaka kukubaliwa, mahakama iliamuru washtakiwa wote kwenda mahabusu mpaka Februali 21, mwaka huu kesi hiyo itakapo tajwa tena.




Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Ziwa, Uthmaan Madati, baada ya kuzindua duka la Tigo, mjini Geita, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Migodi inayolima bangi kufungwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imetishia kufunga migodi midogo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu, ambayo itajihusisha na upandaji wa bangi katika maeneo ya machimbo hayo.

Serikali imesema pamoja na kutambua michango yao mikubwa kwa serikali na jamii zinazozunguka maeneo ya migodi hiyo, lakini kwa tabia iliyoibuka ya kulima zao la bangi maeneo ya migodi midogo haiwezi kuendelea kuvumilika, hivyo itafungwa.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, kwenye mkutano mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa ilani ya chama hicho kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019.

Alisema serikali haitasita kufunga migodi ambayo inatekeleza shughuli za uchimbaji wa madini kinyume cha sheria za nchi hasa kwa kupanda zao la bangi katika maeneo ya migodi, huku wakitambua ni kinyume cha sheria za nchi.

"Mwenyekiti, mimi mwenywe nimeng'oa miche ya bangi kwenye moja ya mgodi mdogo wa madini huko kakola...siwezi kuendelea kung'oa tena miche hiyo, na ili kukomesha tabia ya kulima bangi meneo ya wachimbaji wadogo, ni kufunga migodi itakayobainika kuwa na bangi," alisema Macha.

Aliongeza kuwa vijana wengi kwenye migodi midogo wanavuta sana bangi na mbengu za bangi zinapotapatakaa ndizo zinazoota na kusababaisha maeneo ya wachimbaji kuzungukwa na mimea ya bangi.

"Tutahakikisha tunakomesha tabia hii ili isiendelee na kugeuka maeneo ya wachimbaji kuwa mashamba la bangi."

Aidha, Macha alisema ofisa yake kwa kushirikiana na ofisa ya madini wanaendelea kutambua na kugawa maeneo ya wachimbaji wadogo wa madini maeneo ya Kinamiyumba, Ilindimwime, Buzwagi Bumbiti na Nyangarata.

Alisema kabla ya kuanzisha kwa soko la madini wilayani hapa, walikuwa wakikusanya mrabaha wa serikali kiasi cha ash. milioni 593.6 kwa kipindi cha mwaka mmoja, kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na sasa ambapo wanakusanya kiasi cha Sh. bilioni 10.2 kwa miezi sita pekee.

# Bajeti itilima kukamilisha hospitali, zahanati saba

**Na Happy Severine,** SIMIYU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, imepitisha rasimu ya bajeti ya Sh. bilioni 28.5 kwa mwaka wa fedha 2020/21, ambapo kiasi cha Sh. bilioni 3.9 kati ya hizo, kimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha Halmashauri hiyo imetegemea kutumia kiasi cha Sh. Bilioni 21.7 kwa ajili ya mishahara, Sh. bilioni 1.4 matumizi ya kawaida, huku Miradi ya maendeleo ikiwa ni Sh. bilioni 3.9.

Akisoma rasimu hiyo ya bajeti kwenye kikao maalumu cha Baraza la Madiwani kilichofanyika jana kwa ajili ya kujadili na kupitisha bajeti hiyo, Ofisa Mipango Paul Nyalaja, alisema kuwa Halmashauri hiyo imepanga kukusanya Sh. bilioni 1.4 kama mapato ya ndani.

Alisema katika bajeti hiyo, Halmashauri imeweka vipaumbele muhimu ambavyo ni kukamilisha ujenzi wa zahanati, vyumba vya madarasa shule za msingi na sekondari pamoja na hospitali ya wilaya.

Alisema kuwa Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi imeweka kipaumbele cha ukamilishaji wa zahanti saba ambazo ujenzi wake haujakamilika ili ziweze kutoa huduma.

"Tumetenga kiasi cha Sh. milioni 213.9 ili kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Bulolambeshi, Laini, Mbogo, Songambele, Nkololo, pamoja na Kidulya ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi," alisema Nyalaja.

Aidha, alisema kuwa katika bajeti hiyo wametenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo imefikia kiwango cha asilimia 90 ya ukamilishaji wake.

Aliongeza kuwa hospitali hiyo ni kipaumbele muhimu, ambapo wamepanga kuhakikisha ujenzi wake unakamilika haraka na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Wakijadili bajeti hiyo Madiwani waliipitisha, huku wengi wakisisitiza kuwa nguvu zaidi zielekezwe katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Jackson Skania, Diwani wa Kinamweli, aliwataka watalaamu kuongeza nguvu katika kuhakikisha kila chanzo cha mapato ya ndani kinakusanywa hasa ushuru wa pamba.

"Katika msimu huu wa pamba, Halmashauri yetu ilizalisha pamba nyingi, lakini tumeshindwa kufuatlia kwa karibu bila ya kuogopa ushuru wetu kwenye kampuni zilizonunua, tusipobadilika Halmashauri hii itaendelea kuzalisha madeni," alisema Skania.

Naye Diwani wa Zanzui, William Kuzenza, aliitaka timu ya kukusanya mapato ya ndani kufuatilia kwa karibu magari makubwa ambayo husomba mazao mchanganyiko vijijini kwa mengi yanakwepa ushuru.



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Ziwa Victoria (DMZV), Andrew Gulle, akishirikiana na Mchungaji David Bahn kutoka St. John Cypress, Marekani, kukata utepe kuzindua Shule ya Sekondari ya Mwanza Lutheran, iliyopo jijini Mwanza, juzi. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Waziri Zungu akunwa na utendaji wa NEMC

**Na Mwandishi Wetu,**
DAR ES SALAAM

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu amesifu utendaji kazi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kuahidi kwamba atatumia dhamana aliyopewa kuhakikisha mazingira ya Tanzania yanakuwa salama.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kutembelea ofisi za baraza na kuzungumza na watendaji jana jijini Dar es Salaam, Waziri Zungu amesema licha ya changamoto zilizowasilishwa kwake kupitia mazungumzo na watendaji hao, Baraza limefanya kazi kubwa ya kuhakikisha mazingira yanakuwa mazuri na yasiyoathiri azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda.

"Ninawapongeza NEMC kwa namna walivyofanya kazi katika mazingira yenye changamoto nyingi na wamefanya hivyo bila kuathiri wawekezaji ambao wamekuwa wakijitokeza kwa wingi baada ya kuwa na sera nzuri," ameeleza waziri.

Waziri Zungu amesema kuwa ataongeza nguvu katika mambo yote ambayo watangulizi wake katika Wizara hiyo wameyafanya.

"Nina siku chache tangu niteuliwe katika Wizara hii, lakini kwa namna nilivyoongea na watendaji wa baraza nimepata nguvu ya kusonga mbele kwa ari zaidi huku nikiendeleza mazuri yote ambayo waliopita wameyafanya na mengine yakiwa kwenye mipango endelevu," amefafanua.

Waziri amelezwa kuwa changamoto kubwa ni baraza kutokuwa na mamlaka ya kutosha kusimamia Sheria ya Mazingira na Kanuni zake na Serikali imeombwa ifikirie kuifanya NEMC kuwa namlaka kamili ambayo itaweza kushitaki, kuadhibu na kuamua moja kwa moja bila ya kupitia mlolongo unaofanya utendaji uive.

"Kuifanya NEMC kuwa mamlaka kamili ni jambo muhimu na hatua hii inaweza kuongeza zaidi ufanisi katika utendaji. Changamoto hiyo pamoja na zingine nilizoelezwa nitahakikisha zinafika sehemu sahihi kwa maamuzi ambayo yataweza kulinufaisha zaidi Taifa letu," alisema.

Waziri Zungu ametembelea ofisi hizo za NEMC za Dar es Salaam na Dodoma. Kadhalika amekutana na mabalozi na kuongelea masuala ya mazingira. Mkurugenzi Mtendaji wa NEMC, Dkt Samuel Gwamaka, ameeleza kwamba ziara hiyo imeleta matumaini mapya katika kulifanya Baraza hilo liwe na ufanisi zaidi.

# Wanavijiji wagawiwa majiko banifu bure

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

TASISI isiyo ya kiserikali ya Rukwa Sustainable Development Organization (RUSUDEO), imegawa bure majiko banifu zaidi ya 425 kwa wakazi wa vijiji vya Kazi na Katonto katika Kata ya Lyangalile wilayani Sumbawanga, ukiwa ni mkakati maalumu wa kukabiliana na ukataji miti katika vijiji hivyo.

Akikabidhi jana majiko 425, mkurugenzi wa tasisi hiyo, Divason Abel, alisema kuwa tasisi hiyo ilipata ufadhili kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) kiasi cha Sh. milioni 15,lengo ikiwa ni kutekeleza mradi wa kugawa majiko banifu kwa wananchi wa vijiji hivyo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa majiko hayo yametengenezwa maalumu kwa kuwa yanatumia mkaa kidogo, lengo ikiwa ni kuepusha ukataji miti na uchomaji mkaa ambao umekuwa ni chanzo kikubwa cha kuharibu mazingira.

Alisema majiko hayo hayatumii mkaa mwingi na yanatunza joto ambalo linatumika kwa muda mrefu, hivyo kutumia mkaa kidogo kwa kupika vyakula vingi tofauti na majiko mengine ambayo yanatumia mkaa mwingi.

Ester Luben, mkazi wa Kijiji cha Kazi, alisema kuwa majiko hayo yatawasaidia wanawake waliokuwa wanatumia kuni kama nishati, kwani walikuwa wanakabiliwa na changamoto za kiafya kutokana na moshi unaotoka pindi wanapowasha moto wa kuni kwa ajili ya kupika chakula.

Alisema kuwa wao na watoto wao walikua wanaugua magonjwa ya kifua, kichwa, mafua, macho na kukabiliana na tatizo la kuchelewa kuandaa chakula, kutokana na moto kuwasumbua, hivyo kulazimika kutumia muda mrefu kwa ajili ya kupuliza moto ili uwake. Kaimu mwenyekiti wa Kijiji cha Kazi, Isaya Helman, aliishukuru tasisi hiyo kwa kutekeleza mradi huo katika vijiji vyao kwani utawasaidia wananchi kuondokana na usumbufu wa kutafuta kuni kwani hivi sasa zimekua adimu.

Alisema kuwa serikali inapiga marufuku ukataji miti ovyo kwa lengo la kuhifadhi mazingira, hali iliyosababisha kuni kuadimika na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wanawake wanapoandaa chakula cha familia zao.



# NHC wachangia mifuko 100 ya kukarabati shule

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), mkoani Arusha, limekabidhi msaada wa mifuko 100, ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 1.7 kwa Shule ya Sekondari Felix Mrema, kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya madarasa.

Shule hiyo ipo Kata ya Daraja mbili katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Meneja wa Shirika la Nyumba mkoani Arusha, Ladislaus Bamanyisa, alisema msaada huo wameutoa kutokana na ahadi waliyoahidi mwaka jana shuleni hapo, akiwa mgeni rasmi katika mahafali ya kidato ya nne.

Alisema mifuko hiyo itasaidia kukarabati uchakavu wa sakafu kwenye baadhi ya madarasa.

Shirika hilo limetoa msaada huo, kwa lengo kurudisha faida na gawio waliyopata kwenye jamii .

Bamanyisa alisema shule imejengwa muda mrefu na kukabiliwa na tatizo la uchakavu wa miundombinu ikiwamo sakafu, vyoo pamoja na kupasuka kwa vioo vya madirisha.

"Mifuko hii ya saruji itasaidia kukarabati sakafu za madarasa yaliyochakaa sana, pia tunaahidi kuendelea kutoa msaada zaidi kwa kuwa tukifanya hivi tunamuunga mkono Rais John Magufuli, katika mpango wake wakuboresha sekta ya elimu," alisema Bamanyisa.

Pia aliziomba taasisi nyingine na mashirika mbalimbali kujitokeza kuchangia elimu hususani katika Shule ya Sekondari Daraja mbili, kwa kuwa kufanya hivyo ni mojawapo ya njia ya kuiunga mkono serikali katika jukumu la kuboresha huduma ya elimu.

Mkuu wa shule hiyo, Reginaldo Msendekwa, amelishukuru shirika hilo, kwa msaada huo utakaopunguza baadhi ya matatizo kwenye shule.

NHC pia walitoa Sh. milioni mbili kwa ajili ya ukarabati wa vioo vya madirisha ya madarasa.

Mjumbe wa Bodi ya shule hiyo, Hussein Dudu, amelishukuru shirika hilo kwa msaada huo.



Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini wa Taasisi ya kulea watoto yatima ya SOS International Tanzania, Dk. Mary Nagu, akipanda mti wa kumbukumbu katika uzinduzi rasmi wa shule ya watoto yatima iliyokuwa ikisimamiwa na SOS, ambayo sasa inafadhiliwa na kuongozwa na Mfuko wa kusaidia elimu wa Kimataifa wa Uturuki wa Turkish Maarif Foundation (TMF), eneo la Ngaramtoni, mkoani Arusha juzi. Kulia kwake ni Mkuu wa kituo cha shule hizo, Herry Salum na Balozi wa Uturuki hapa nchini, Ali Dovutoglu na wadau wengine. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## CCM yaridhishwa utekelezaji Ilani

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Arumeru wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani humo.

Wajumbe wa Kamati ya Siasa, walifanya ziara ya kutembelea miradi ya maendeleo katika Tarafa ya Moshono, kama sehemu ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Wajumbe hao, wameridhishwa na ubora wa ujenzi wa miradi waliyoikagua na walithibitisha kuona mapinduzi ya kimaendeleo yaliyofanywa na serikali kwa wananchi wa vijijini kwa kipindi cha miaka minne.

Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Arumeru, Simon Ole Saning'o, amesema ameona mapinduzi makubwa ya kimaendeo, yaliyofanywa na serikali kwa wananchi kwa kipindi cha miaka minne chini ya Rais John Magufuli.

Saning'o alisema Serikali imetekeleza Ilani ya CCM kwa zaidi ya asilimia 90, kwa kujenga miradi mikubwa katika sekta za elimu, afya, maji, umeme, pamoja na miundombinu ya barabara.

Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Sokoni II, ujenzi uligharimu kiasi cha Sh. milioni 190, kwa ufadhili wa Ubalozi wa Japan hapa nchini.

Mradi mwingine uliotembelewa ni wa maktaba na ukarabati wa bwalo katika Sekondari ya Mlangarini uliogharimu Sh. milioni 140, pia ujenzi wa darasa moja katika Shule ya Sekondari Olokii kwa nguvu za wananchi, ujenzi wa kituo cha afya Nduruma, Sh. milioni 500, fedha hizo zilitoka Serikali Kuu.

# Shirika kuwakomboa watoto wa kike dhidi ya 'mafataki'

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Cosita, limejipanga kuwakomboa watoto wa kike kwa kuwajengea mabweni ili waepuke vishawishi kutoka kwa mfataki wakati wakienda shuleni.

Kadhalika limejipanga kuihamasisha jamii katika halmashauri kujenga mabweni kwa wanafunzi wa kike wa shule za msingi wilayani humo, ili wanafunzi hao wasitembee umbali mrefu.

Hayo yalisemwa jana mjini Babati na Mkurugenzi wa Cosita, Patrice Gwasma, wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo la kuwaeleza mpango mkakati waliyojiwekea kusaidia kuhamasisha ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wa kike. Pia, alisema wameanza kufanya uhamasishaji wa ujenzi wa mabweni kwa watoto wa kike katika shule za sekondari, baada ya kubaini kuwa wengi wa wanafunzi wanakatisha ndoto zao kwa kurubuniwa na wanaume wakati wa kwenda shule na kurudi.

Alisema mpango huo, wataanza kuutekeleza kwa Shule ya Sekondari Sigino, ambayo wanafunzi wa kike wanatembea kilomita sita hadi 10, kwenda shuleni na kurudi nyumbani. Mkuu wa Shule ya Sekondari Sigino, Mwalimu Augusino Burra, alisema wanafunzi hao wanatoka katika vijiji vya Sigino, Daghailoi saba, Imbilil, na kijiji cha Wangbay. Hata hivyo, alisema wanafunzi walioacha shule kwa kupata ujauzito ni watano, mwaka 2016 wanafunzi ni wawili, 2017 mwanafunzi mmoja, mwaka 2018, mwanafunzi mmoja na mwaka 2019 ni mwanafunzi mmoja.

Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Mji wa Babati Pascalina Lowokelo, alisema ni mwanzo mzuri kwa Shirika la Cosita kuleta ukombozi kwa watoto wa kike.

"Watoto wote wanatakiwa kulindwa, lakini linapokuja suala la mtoto wa kike linahitaji ulinzi zaidi kwa sababu wao hupitia mambo mengi tofauti na wa kiume," alisema. Alisema juhudi za Cosita zitasaidia kupunguza tatizo la mimba za utotoni, pia kuongeza ufaulu kwa watoto wa kike na maumivu kwa wazazi ya kusomesha mtoto na baadaye kukatisha masomo kutokana na kurubuniwa.

Takwimu za utafiti wa idadi ya watu na afya Tanzania za mwaka 2015/2016 zinaonyesha kuwa asilimia 27 ya wanawake vijana wenye umri wa miaka 15, hadi 19 wana watoto na wengine ni wajawazito .

# Viongozi wa kimila walalamikiwa kuficha siri

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WANAWAKE wa jamii ya wafugaji wa Kimasai katika Kata ya Ruvu, Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, wamelalamikia viongozi wa mila katika ngazi ya vijiji kuhongwa ng'ombe ili kuficha siri kwa viongozi wa serikali wanaofuatilia watoto wa kike wanaoozeshwa katika umri mdogo.

Kiongozi wa wanawake mashuhuri wa Kimasai ambaye ni mjumbe wa Jukwaa la vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo) la Wilaya ya Same, Rehema Majuka, alisema idadi ya wasichana wa jamii hiyo wanaoendelea kuchumbiwa kabla ya kuhitimu darasa a saba na kidato cha nne inaongezeka kutokana na rushwa ya mifugo inayotolewa kwa viongozi wa mila.

"Hapa kwetu Ruvu, wazee wa mila wanamchukulia mwanamke ni mtu ambaye hana maamuzi wakimwita Ngerai, kwa lugha yetu yaani wakimfananisha na mtoto ambaye hana maamuzi.

"Watoto wa kike wa Kimasai bado wanaolewa kwa kasi ya ajabu, na hilo linasababishwa na wazee wetu wa mila ambao wanapokea zawadi ya ng'ombe kutoka kwa wazazi wanaoozesha watoto wao. Lakini pia ukeketaji nao uko kwa kasi hiyo hiyo, ndio maana tunaomba mamlaka za serikali kuchunguza na kuchukua hatua kali."

Alisema baada ya wazee wa mila kupokea ng'ombe ili kuficha siri kwa ajili ya kuwalinda wazazi, mama mwenye mtoto anayeolewa hivi sasa na yeye anahongwa kiasi cha Sh. 300,000 ili kutoa baraka kwa mwanae kuondoka nyumbani.

Alipotafutwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, kujua iwapo serikali ina taarifa kuhusu ukatili huo unaoendelea Kata ya Ruvu, alisema tayari maofisa ustawi wa jamii na makachero wa polisi wanafuatilia malalamiko hayo ya wanawake wa kata hiyo.

Zaidi ya wanawake 4,000 wa Mkoa wa Kilimanjaro, hivi sasa wanaandaliwa kutumika kama askari kanzu wa kuchimba na kuibua matukio ya ukatili wa kijinsia yanayotishia ustawi wa jamii katika halmashauri saba za mkoa huo kwa sasa.

Kwa mujibu wa Mratibu wa mradi ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto wa Mkoa wa Kilimanjaro, Veronica Ullomi, lengo hasa ni kuwaelimisha kwanza kutambua ukatili wa kijinsia upo, lakini pia mikakati na mbinu gani wanayoweza kutumia ili kupambana na matukio hayo.

"Hivi sasa tunatoa elimu ya jinsi ya kuendelea kuwakagua watoto wetu, watoe taarifa kama kuna matukio ya ukatili, lakini wachukue hatua ya kuielimisha jamii jinsi ya kukabiliana na matatizo haya.

"Hawa watakuwa ni wawakilishi wa wanawake wengine, kwa sababu hao wanatoka kwenye makundi mbalimbali ya ujasiriamali, majukwaa ya wanawake katika kila wilaya, vyama vya watu wenye ulemavu na wanawake mashuhuri ambao watatumika kuwaelimisha wanawake wengine kwenye ngazi ya chini zaidi," alisema Ullomi.

# Udahili wakwamisha wanafunzi kujiunga OUT

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

IDADI ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaojiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kila mwaka inazidi kushuka huku sababu kubwa ikitajwa kuwa mfumo wa udahili 'kukibana' kwa kuweka vigezo vinavyofanana na vyuo vikuu vingine.

Mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi wa chuo hicho, Prof. Elfas Bisanda, alisema katika nchi zenye vyuo vikuu huria hasa Afrika na katika mabara mengine, Tanzania ndio pekee yenye idadi ndogo ya udahili wa wanafunzi wanaojiunga na chuo hicho.

Prof. Bisanda alikuwa akizungumza jana na wafanyakazi wa chuo hicho kutoka Tanzania Bara na Visiwani katika Manispaa ya Moshi.

"Wakati Tanzania ikiwa na wanafunzi 69,000 waliodahiliwa kujiunga na vyuo vikuu, nchi ya China inaongoza kwa udahili wa wanafunzi zaidi ya milioni tano, ikifuatiwa na India yenye wanafunzi milioni tatu, huku Afrika Kusini ikiwa na wanafunzi 450, 000," alisema.

Mwaka jana, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), iliainisha sifa zinazohitajika ili kuwawezesha waombaji kupata nafasi ya kusoma katika vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Udahili wa kujiunga na shahada ya kwanza utahusu waombaji waliohitimu wa kidato cha sita, wenye Stashahada (Ordinary Diploma); na waliomaliza programu ya 'Foundation' ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Awali akitoa salamu zake, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliwataka kuwa na mipango chanya itakayofanya chuo hicho kuwa endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa upande wake, Ofisa Kazi Mkoa wa Kilimanjaro, Mwinyimkuu Mtulia, amewataka wafanyakazi hao kufuata sheria za kazi ili kuepuka migogoro ambayo imekuwa ikisababisha baadhi ya wafanyakazi kukosa haki zao.




Kiongozi wa wanawake mashuhuri wa jamii ya wafugaji wa Kimaasai kutoka Kata ya Ruvu, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Rehema Majuka (kushoto), akitoa maelezo kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia kwa jamii hiyo, mbele ya kamati ya mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wilayani humo jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Madaktari bingwa wabaini Siha kuwa na tatizo la macho

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

RIPOTI ya uchunguzi wa jopo la madaktari bingwa kutoka mikoa mbalimbali nchini waliokuwa wakifanya uchunguzi wa tatizo la magonjwa ya macho katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wamegundua wananchi 1,450 wanakabiliwa na maradhi hayo na wanahitaji tiba haraka ikiwamo kufanyiwa upasuaji.

Jana, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Andrew Method, alithibitisha kuwa wananchi 1,450 waliohudhuria kambi maalumu ya uchunguzi wa maradhi hayo, ndio waliogundulika wana tatizo na wanahitaji tiba.

"Asanteni sana Lions Club (Dsm & Moshi), Pfk na kampuni ya uzalishaji wa parachichi ya Africardo kwa kuwezesha huduma ya macho ikihusisha uchunguzi, tiba, miwani na upasuaji.

"Pia katika kambi hiyo, tulifanya uchunguzi mwingine wa magonjwa ya shinikizo la damu na ugonjwa wa kisukari kwa wakazi zaidi ya 1,900 katika Wilaya ya Siha, tutakuja na ripoti yake siku chache kuanzia sasa na umma utaelezwa kama kuna tatizo."

Kwa mujibu wa Dk. Method, shinikizo la damu sasa ni tishio jipya kwa wakazi wa Wilaya ya Siha ambalo ni kati ya magonjwa 10 yanayowasumbua wananchi wa eneo hilo. Alisema rekodi za afya wilayani humo zinaoyesha kuwa shinikizo la juu la damu, sukari na magonjwa ya macho ndio tatizo kuu linalowasumbua wakazi wa Siha kwa miaka mitano iliyopita.

"Rekodi zetu zinaonyesha kwamba shinikizo la damu, sukari na magonjwa ya macho ni kati 10 yanayosumbua Siha kwa kipindi ha miaka mitano sasa," alisema Dk. Method.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wananchi namna ya kujilinda ili kuepuka kupata magonjwa hayo, kwa kuwa yanaweza kuzuilika endapo wananchi watapata elimu.

Kutokana na hali hiyo, amewashauri wakazi wa wilaya hiyo kuzingatia mazoezi ili kuwa na miili yenye ubora na kushindwa kupata magonjwa ya mara kwa mara.

Awali, mmoja wa wafadhili wa kambi hiyo ya matibabu ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Kilimo cha parachichi ya Africado, James Person alisema zaidi ya Sh. milioni 20 zimetumika kugharamia matibabu hayo.

# ama

ALHAMISI FEBRUARI 20, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Madaktari: mwanzilishi Weakleaks anateswa kiafya**



Ukurasa 16

Ndivyo kifafa kilivyo na matibabu yake



Ukurasa 17

## Bangi hii ni shida kweli namna hii



# Mtafiti Taasisi Ifakara afukua mazito ya kichaa cha mbwa

Ukurasa 18



Mwanzilishi Mtandao Wikleaks, Julian Assange. **PICHA: MTANDAO.**

## Madaktari: Mwanzilishi Weakleaks anateswa kiafya

MADAKTARI zaidi ya 100, pamoja na Shirika la Kutetea Haki za Waandishi wa Habari duniani, wanasema mwanzilishi wa mtandao wa Wikleaks, Julian Assange, anayeshikiliwa nchini Uingereza, anateswa kisaikolojia.

Barua iliyoandikwa na madaktari na shirika hilo, wiki moja kabla ya Mahakama ya Uingereza kuanza kusikiliza kesi ya Assange, ina malalamiko ya kutopewa huduma bora za kiafya na huenda itaamuliwa apelekwe nchini Marekani kujibu mashtaka ya ujasusi.

Pia, Shirika la Waandishi Habari Wasiokuwa na Mipaka (Reporters Sans Frontieres), kimelaani mateso ya kisaikolojia anayofanyiwa kiongozi huyo wa WikiLeaks kwenye barua ya pamoja iliyotangazwa kwenye gazeti la kitabibu la Uingereza, The Lancet.

Kundi hilo la madaktari 117 kutoka nchi 18 wameituhumu serikali ya Uingereza, wiki moja tu kabla ya mahakama, kuanza kusikiliza kesi ya kupelekwa Marekani kwa raia huyo wa Australia mwenye umri wa miaka 48.

Asange, anashikiliwa kwenye gereza lenye ulinzi mkali la Belmarsh, Kusini mwa jiji la London na Mjumbe wa Umoja wa Mataifa, Nils Melner, anatoa angalizo la madhara kwa Asange.

Tangu mwaka wa 2015, Assange alifanyiwa uchunguzi na daktari kwenye ubalozi wa Equador alikokimbilia kwa miaka mitatu, kabla ya mapendekezo ya madaktari wake kupewa huduma bora ya kiafya yanadaiwa kupuuzwa. **DW**

MAZINGIRA

# Wakala TFS kunyakua matunzo msitu muhimu wilayani Chunya

## • Chanzo maji Ziwa Rukwa, Mto Ruaha • Katika mchakato kuwa Hifadhi rasmi • Mkoa wafurahia, waipa wakala ruksa



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), pamoja na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa, wakiangalia ramani ya Msitu wa Kambikatoto wilayani Chunya ambao Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) unakusudia kuuhifadhi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

**Na Nebart Msokwa,** Mbeya

MSITU wa Kambikatoto unaopatikana katika Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya unakabiliwa na uharibifu unaosababishwa shughuli za kibinadamu. Hapo zinatajwa shughuli za kilimo, ufugaji na uvunaji holela wa miti.

Athari za mahali hapo, kwenye kata mbili za Kambikatoto na Mafyeko zenye vijiji vya Kambikatoto, Bitimanyanga, Mafyeko na Lualaje, viko umbali wa kilomita 160 kutoka Chunya mjini, vivyo hivyo kilomita 232 kutoka Mbeya Mjini, katika barabara kuu ya Mbeya - Tabora.

Hifadhi hiyo na Hifadhi ya Nyuki ya Kipembawe, ziko chini ya Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS).

Vilevile, upande wa Magharibi Msitu huo unapakana na Pori la Akiba la Rukwati/Piti linalosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (Tawa) na upande wa Mashariki, inapakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

> **Endapo watafanikiwa kuuhifadhi msitu huo, utakuwa ndio mkubwa kuliko misitu yote ambayo inasimamiwa na TFS katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.**

Taarifa za wataalamu wa Misitu, zinaonyesha kuwa uoto wa asili wa msitu huo, ni miti ya miyombo japo kuna mingine kama Malama (Combretum SP), Misaula (Perinari SP), Mitondoro na Migunga (Acacia Sp).

Baadhi ya maeneo ya msitu huo yamevamiwa na kuharibiwa na wananchi wanaoendesha shughuli zao kutokana na usimamizi wa vijiji vinavyouzunguka kuwa mdogo, hivyo kuruhusu msitu kuingliwa.

Baadhi ya wanachunga mifugo ndani ya msitu, wengine wanaendesha shughuli kilimo na baadhi wanavuna miti kwa ajili ya kupasua mbao, kuni za kupikia na wengine wanachoma mkaa, hivyo kuhatarisha msitu huo kutoweka.

Kutokana na hali hiyo, TFS wameingilia kati na kuanza harakati za kuuhifadhi, ili kuokoa rasilimali mbalimbali zilizomo kwa ajili ya vizazi vya sasa na baadaye.

### SABABU NINI?

Kaimu Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, anasema msitu huo una ukubwa wa zaidi ya Hekta 179,078 lakini linalofaa kuhifadhiwa lina ukubwa wa hekta 100,008 kutokana na umuhimu wake

Anasema msitu huo ni muhimu kuhifadhiwa, kwa sababu ndio ushoroba (mapitio ya wanyamapori) unaounganisha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Pori la Akiba la Rukwati/Piti ambalo lipo upande wa Wilaya ya Songwe.

Lupembe anasema, kutokana na uharibifu unaoendelea kukifanyika, umesababisha hata mtiririko wa wanyama kupita umebadilika, hivyo unahatarisha ustawi wa hifadhi hizo muhimu kwa taifa.

Aidha, anautaja msitu huo ni chanzo cha maji kutokana na mito inayotiririsha maji kuelekea kwenye Ziwa Rukwa na Mto Ruaha Mkuu, ambao ni muhimu kwa kilimo na uzalishaji wa umeme, hasa katika zama zilizopo kuelekea kwenye uchumi wa viwanda.

"Baadhi ya mito ambayo vyanzo vyake vipo ndani ya Msitu huu ni Mpaka, Sipa, Piti, Mlungwiji, mwiji, Ilama na Mzombe, pia huu msitu una uoto mwingi ambao unawezesha ufugaji wa nyuki na una bioanuai muhimu za miti na wanyama," anasema Lupembe.

Hata hivyo anasema TFS inataka kuuhifadhi msitu huo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo ni tishio kwa jamii duniani katika miaka ya sasa.

### HATUA ILIYOFIKIWA

Lupembe anasema, sheria ya misitu namba ya Mwaka 2002, unataja hatua tisa za kufuata wakati wa kuhifadhi misitu mipya na kwamba kati yake, sita wameshazikamilisha na sasa wanaendelea kukamilisha tatu.

Anataja baadhi yake ni kutambua eneo linalotakiwa kuhifadhiwa, kuchunguza mipaka ya msitu unaotakiwa kuhifadhiwa kwa kushirikiana na maofisa na wanavijiji wanaozunguka msitu husika.

Hatua zingine alizotaja, ni makubaliano na wanavijiji kuhusu mipaka itakayoridhiwa na pande zote, kisha wanaandaa muhtasari wa makubaliano unaoambatana na sahihi za wenyeviti wa vijiji, kuwasilisha mihutasari wilayani kwa ajili ya kupata maoni.

Vilevile anasema, baada ya hatua hiyo kukamilika, iliandaa muhutasari ulioambatana na sahihi ya Mkuu wa Wilaya, kisha eneo likapimwa kwa mujibu wa sheria na ramani yake ikachorwa kulingana na makubaliano.

"Kwa mujibu wa sheria Muhtasari wa wilaya unatakiwa kuwasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na kisha makubaliano ya kamati yanaambatana na saini ya Mkuu wa Mkoa kwenye fomu maalumu na hii ndiyo hatua tuliyofikia," anasema Lupembe.

Hata hivyo anasema, hatua zilizobakia ni tatu pekee ambazo ni kuwasilisha nyaraka zote makao makuu ya TFS, kutangazwa kwenye gazeti la serikali na ya kuuhi-

MAZINGIRA

# Wakala TFS kunyakua matunzo msitu muhimu wilayani Chunya

fadhi, ili kuutambulisha kwa wananchi kwa muda wa siku 90 na kama hakuna malalamiko, utangazwe rasmi kuwa msitu wa hifadhi.

Lupembe anasema endapo watafanikiwa kuuhifadhi msitu huo, utakuwa ndio mkubwa kuliko misitu yote ambayo inasimamiwa na TFS katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

**MBUNGE MWAMBALASWA**

Novemba 27 mwaka jana, maofisa wa TFS katika azma yao ya kuuhifadhi msitu huo kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), ambacho Mbunge wa Jimbo la Lupa wilayani Chunya, Victor Mwambalaswa alikuwa mjumbe aliyehudhuria.

Katika hoja hiyo, Mwambalaswa ambaye msitu huo upo ndani ya eneo lake, aliiomba kamati iridhie kwa maelezo kuwa, msitu una umuhimu mkubwa katika hifadhi ya mazingira.

Anataja misitu mingine wilayani humo, nayo ina umuhimu mkubwa, ikiwemo kusaidia kuwepo mvua ya kutosha katika mkoa Mbeya na jirani.

Mwambalaswa anasema, Chunya ndio ina misitu mingi iliyohifadhiwa, ikilinganishwa na wilaya zote za Mbeya na kwamba, faida yake inaonekana, huku akipongeza TFS kwa wazo hilo.

"Sisi tunaotoka kwenye maeneo yale ndio tunaojua umuhimu wa msitu ule. Dunia nzima sasa hivi inahubiri mabadiliko ya tabianchi, sasa hii ni fursa kubwa kwetu wananchi wa mkoa Mbeya maana sisi ndio wanufaika wa kwanza wa misitu hii," anasema Mwambalaswa.

"Wajumbe turidhie msitu huu uhifadhiwe, kwa sababu wenzetu hawa tayari wameshafuata taratibu na sisi kazi yetu ni kushauri na kupitisha mambo muhimu," anasema Mwambalaswa.

**MADIWANI CHUNYA**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, ni miongoni mwa wajumbe walioambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama, kutembelea mipaka ya msitu huo hivi karibuni na anakiri halmashauri yake kupokea muhtasari wa vijiji vinavyozunguka msitu huo.

Mwanginde anaeleza kutokana na uhalisia, hakuna haja ya kupinga wazo la TFS na kutokana na muhtasari wa vijiji uliowasilishwa, Halmashauri ilibaini wananchi walishirikishwa vizuri na waliridhia kukabidhi msitu kwa TFS.

"Tungepokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka kwamba taratibu hazikufuatwa, tungeshauri zoezi lisitishwe kwa sababu ingeibua migogoro mingi. Sasa wananchi wenyewe waliridhia hivyo nasi tunaungana na wananchi wetu,"



Wananchi wa Kata ya Kambikatoto, Chunya wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (hayupo pichani) alipokuwa anazungumza nao kuhusu Hifadhi ya Msitu wa Kambikatoto, unaokusudiwa kuhifadhiwa na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS). **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

> **Sisi tunaotoka kwenye maeneo yale ndio tunaojua umuhimu wa msitu ule. Dunia nzima sasa hivi inahubiri mabadiliko ya tabianchi, sasa hii ni fursa kubwa kwetu wananchi wa mkoa Mbeya maana sisi ndio wanufaika wa kwanza wa misitu hii.**



Moja ya misitu iliyovamiwa wilayani Chunya. **PICHA: MTANDAO.**

alisema Mwanginde.

Diwani wa Kata ya Kambikatoto ulipo msitu huo, Christopher Mchafu, anakiri wananchi wake walishirikishwa katika hatua zote za kuuhifadhi na kwamba walipewa kwanza elimu juu ya umuhimu wa kuhifadhiwa kwa msitu huo.

Anasema vijiji vyote viliunda kamati maalumu za kushirikiana na maofisa wa TFS na hata mikutano ya hadhara iliyokuwa inalenga kusikiliza maoni ya wananchi ilifanyika ya kutosha.

**WANANCHI NAO**

Baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo, wanakiri kuwa msitu huo ukiwa chini ya TFS utasimamiwa vizuri kutokana na maofisa wa taasisi hiyo kuwa na elimu ya uhifadhi tofauti na wao ambao wamekuwa wakiisimamia bila kuwa na elimu.

Mmoja wa wananchi hao, Lucian Lazaro, anasema wao walikuwa hawawezi kudhibiti uharifu ndani ya msitu huo kwa sababu wana nyenzo za kuwasaidia kufanya doria kwenye maeneo yaliyokuwa yanavamiwa.

Anasema kitendo cha TFS kuamua kuhifadhi kinawasaidia wao wenyewe kwa maelezo kuwa wao ndio watakaokuwa wananufaika zaidi na msitu huo kuliko maofisa wa TFS ambao baadhi sio wenyeji wa Mkoa wa Mbeya.

"Sisi tumeridhia kwa moyo wote hawa wenzetu wauchukuwe msitu huu na kuuhifadhi, lakini maombi yetu kwao ni kwamba waendelee kuheshimu mipaka tuliyokubaliana ili kuepuka kuibua migogoro baadaye," anasema Lazaro.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo, aliyeambatana pia na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwenda kukagua mipaka ya msitu huo, anawasihi wananchi kutunza mazingira.

Anasema, misitu iliyopo wilayani Chunya, ukiwemo na wa Kambikatoto, ni miongoni mwa sababu ya mkoa Mbeya kuwa na hali nzuri ya hewa, inayoruhusu mazao mbalimbali kustawi.

Dk. Mwakajumilo anasema, ili neema hiyo iendelee kuwapo miaka mingi, ni vyema wananchi wakakaa mstari wa mbele kutunza misitu iliyopo, TFS ikiendelea kuheshimu mipaka.

"Hivi karibuni Rais Magufuli alifuta baadhi ya mapori na kupunguza baadhi ya maeneo ya hifadhi, ili kupunguza migogoro ya ardhi. Sasa ili tuihifadhi kwa ufanisi misitu hii, wenzetu TFS lazima mheshimu mipaka yenu," alisema Dk. Mwakajumilo.

**RC CHALAMILA**

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyeongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa kukagua msitu huo, alisema ameridhishwa na taratibu zilizofuatwa na maofisa TFS kuhifadhi msitu huo.

Chalamila alisema ili kuhakikisha Msitu huo unakuwa salama zaidi, Serikali inakusudia kujenga Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Gereza, taasisi ambazo zitasaidia kwenye ulinzi wa rasilimali za Msitu huo.

"Huu msitu tungekuwa tunamuuzia mtu binafsi ingekuwa tatizo lakini sasa tunataka kuuhifadhi sisi wenyewe, ikitokea serikali ikataka kubadili matumizi na kuyatumia maeneo haya kwa shughuli zingine inakuwa rahisi kuyachukua hivyo tushirikiane kuyatunza," anasema Chalamila.

Anawataka wananchi wote wa mkoani Mbeya, kuepuka kukata miti ovyo kwa maelezo kuwa wataharibu uoto wa asili na kuhatarisha maisha yao wenyewe kwa kujiletea jangwa.

AFYA

# Ndivyo kifafa kilivyo na matibabu yake

## • Bugando rasmi sasa kuhudumia • Orodha ya vyanzo vyake halisi

**Na Mary Geofrey**

KIFAFA ni ugonjwa unaotokana na hitilafu au jeraha kwenye ubongo linalosababisha mgonjwa kuanguka, kukakamaa, kuzimia au kutozimia na wakati mwingine kutoa povu mdomoni.

Nchini ugonjwa huo umekuwa ukihusishwa na imani za kishirikina, jambo linalosababisha watu kushindwa kuwahi hospitali kupata matibabu.

Wakati jamii ikiamini ni imani potofu, madaktari wao wanasisitiza ugonjwa huo hutokea kwa sababu ya hitilafu za neva ambazo hutokea ghafla na kuisha ghafla.

Daktari Bingwa wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Patience Njenje, anaelezea kwa kina kuhusu ugonjwa huu, sababu, takwimu na namna wanavyotoa tiba nchini.

Anasema duniani watu wanaoishi na kifafa wako zaidi ya milioni 60 na bara la Afrika ndilo limeathirika na tatizo hilo, liko zaidi kwa watu wenye umri kati ya miaka 20 hadi 50, huku Tanzania kukadiriwa kuwa na wagonjwa milioni moja.

"Wanaoishi na tatizo la kifafa wako katika hatari ya kifo mara sita zaidi ukilinganisha na jamii yote kwa ujumla.Wagonjwa wengi wa kifafa ni vijana, wakiwa na umri wa wastani wa miaka 15," anasema Dk. Njenje.



Wakazi wa Manzese wakifuatilia elimu kuhusu kifafa iliyotolewa na madakatari bingwa wa Ubongo, Uti wa Mgongo, Mishipa ya Fahamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### IMANI POTOFU

Anasema, idadi kubwa ya watu nchini wana imani potofu kuhusu kifafa na kwamba zaidi ya asilimia 36 ya watu bado wanaamini kuwa ugonjwa wa kifafa unatokana na nguvu za giza.

Dk. Njenje anasema, zaidi ya asilimia 50 ya wana jamii bado wanaamini kuwa kifafa ni ugonjwa wa kuambukiza hivyo huwanyanyapaa wagonjwa na kuwasababishia msongo wa mawazo na kukosa furaha.

Anaendelea kusema kuwa zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa kifafa nchini huenda kutafuta tiba kwa waganga wa kienyeji na viongozi wa dini wakiamini mgonjwa amevamiwa na 'mapepo' mabaya au mashetani.

Kwa mujibu wa Dk, Njeneje asilimia 60 ya wagonjwa wanaofika kupata tiba hospitalini hufika mwaka mmoja baada ya kupata tatizo: "Ni kati ya asilimia tano hadi 10 ya wagonjwa wa kifafa Tanzania ndio hupatiwa matibabu hospitalini, hivyo wengi wanaoishi na kifafa Tanzania wana kifafa ambacho ni cha kiwango cha juu."

### SABABU ZAKE

Dk. Njenje anasema chanjo ni homa kipindi cha utoto, ambazo chanzo chake huwa ni magonjwa kama malaria yanayomsababisha mtoto kupata degedege na athari zake ni pamoja na kupata jeraha kwenye ubongo linalosababisha kifafa.

Anasema, pia ajali zinaweza kumsababishia mtu kifafa, kwa kuwa mtu anapopata ajali hupata majeraha ya ndani, ikiwamo kwenye ubongo bila yeye kujua na athari zake hutokea miaka mingi baadaye.

> **Ni muhimu kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya juu ya chanzo, jinsi ya kujikinga na matibabu sahihi kwa watu wenye kifafa.**

Dk. Njenje anasema, pia matatizo ya kipindi cha ujauzito na wakati wa kujifungua, yanaweza kumsababisha mtoto kuchelewa kupata hewa ya oksijeni na mtoto akapata jeraha kwenye ubongo linalomsababishia kifafa.

Anasema, pia minyoo sugu au inayosababishwa na upungufu wa kinga, mwilini huweza kupanda kichwani na kuleta hitilafu.

Dk.Njenje anasema ugonjwa wa kifafa umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza hitilafu inapotokea katika sehemu moja ya ubongo, humfanya mgonjwa asipoteze fahamu ila anaweza kuwa hafahamu anachokifanya.

Anasema, hitilafu inatokea kwenye ubongo unaoendesha vitendo na dalili zake zinaweza kuwa kutetemeka kwa sehemu moja ya mwili kama kidole, mkono wote, upande mmoja wa mkono na mguu, upande mmoja wa uso.



Baadhi ya madaktari wa Hospitali ya Rufani Bugando, wakijadili jambo kuhusu tiba ya kifafa.

Anasema kama hitilafu itatokea kwenye ubongo unaoendesha hisia kama harufu au usikivu dalili zake zinaweza kuwa kusikia harufu au kelele ambazo kiuhalisia hazipo.

Dk. Njenje anasema, kama hitilafu itatokea kwenye sehemu ya ubongo unaoendesha kufikiri au kuongea, mtu ataanza kuongea au kucheka ovyo au kubadilika kwa hali ya mapigo ya moyo

Kuhusu sehemu ya pili ya ugonjwa wa kifafa ni hitilafu inapotokea katika sehemu mbili za ubongo, dalili hizi hutokea na mgonjwa hupoteza fahamu.

Anasema anaanguka na kugeuza macho juu, kutetemeka mwili mzima pengine na kutoa povu na kwamba ndiyo dalili ya kifafa ambayo wengi huona inatisha.

Daktari huyo anasema, anayeanguka anajigonga hasa kwa watoto na kuzubaa au kuacha anachokifanya na kuwa kama anaota, hali ambayo hutokea mara nyingi na huwatokea zaidi watoto.

"Ukipata au kushuhudia mtu anapata dalili hizi ni muhimu kupelekwa kituo cha afya, ili uchunguzi ufanyike na kupewa matibabu ya kuzuia dalili za kifafa na kutibiwa ugonjwa huu ulioathiri ubongo," anasema Dk. Njenje.

Anatumia fursa hiyo kuwataka wananchi kujikinga na visababishi vinavyozuilika, kama kumjali mama mjamzito kipindi cha ujauzito kwa kumshauri kuhudhuria kliniki, pamoja na kumpatia vipimo kila mara.

Pia, anasema ni muhimu kufanya uchunguzi na watoto kupata matibabu ya haraka kwa watoto wanaopata homa, matumizi ya choo, kunawa mikono na kula nyama ya nguruwe iliyoiva.

Anawataka wadau washirikiane kutoa elimu ngazi zote za kijamii ili kuondoa unyanyapaa kwa watu wenye matatizo ya kifafa. Dk. Njenje anasema:"Ni muhimu kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya juu ya chanzo, jinsi ya kujikinga na matibabu sahihi kwa watu wenye kifafa."

### BUGANDO WATIBU

Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, mkoani Mwanza, imekuwa ikitoa huduma za kibingwa za matibabu ya kifafa, kwa watoto na watu wazima kwa kutumia mashine za kisasa.

Katika ziara ambayo Nipashe ilikuwamo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilikutana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Bahati Wajanga, anayesema huduma hiyo ilianza kutolewa mwaka jana, baada ya hospitali hiyo kununua mashine maalum ijulikanayo kama EEG yenye uwezo wa kubaini ugonjwa huo.

Anasema tangu kuanzishwa huduma hiyo imefanikiwa kutibu wagonjwa 600 wanaosumbuliwa na maradhi hayo na Bingwa wa Tiba ya Watoto, Mishipa ya Fahamu na Ubongo, Dk. Yusuph Jamnagerwalla, anasema mashine hiyo inachukua vipimo vya mgonjwa ndani ya saa mbili na kutoa majibu ndani ya saa siku moja hadi mbili.



Profesa William Matuja wa Chuo Kikuu Kishiriki Cha Sayansi na Tiba (MUHAS) na Rais wa Chama Cha Wagonjwa wa Kifafa nchini (TEA).

"Mashine hii ina uwezo wa kupima na kubaini ugonjwa huu ndani ya saa mbili na mgonjwa ataanzishiwa matibabu mara moja na kuna uwezekano wa kupona kuanzia wiki 14 hadi mwezi mmoja," anasema Dk. Jamnagerwalla.

Kuhusu sababu za kuwapo kwa ugonjwa huo, anasema walifanya utatafiti mdogo na kubaini kati ya watu kila watu 100 wenye mtindio wa ubongo, asilimia 60 wanaugua kifafa.

Anasema pia watoto waliozaliwa na tatizo la ubongo wapo kwenye hatari ya kupata ugojwa wa degedege, hususani walaji wa nyama ya nguruwe ambayo haijaiva vizuri, kwani ina virusi vinavyosababisha kifafa.

> **Pia minyoo sugu au inayosababishwa na upungufu wa kinga, mwilini huweza kupanda kichwani na kuleta hitilafu.**

Dk. Jamnagerwalla, anataja sababu nyingine ni kama walizotaja Muhimbili, kwamba ni ajali zinazosababisha ugonjwa wa kifafa, baada ya kupata majeraha kwenye ubungo.

Anasema sasa wanatoa elimu kwenye vituo vya afya na zahanati mkoani humo, kuwasihi watu wenye ugonjwa huo kujitokeza kupima na kuanza matibabu kwa sababu unatibika na kwamba wanaendelea kutoa elimu hadi shuleni.

Anasema, awali kabla ya kuwa na mashine hizo za kisasa, wagonjwa walilazimika kwenda Muhimbili, hivyo imewapunguzia gharama kwa wagonjwa wa Kanda ua Ziwa.

# Bangi ni shida kweli namna hii



Uvutaji bangi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Juster Prudence**

KIPO kilio cha umma kuhusiana na watu kuendekeza uvutaji bangi na hata imekuwa ya kihistoria. Labda kuna swali la msingi hapo kujiuliza, bangi ni nini?

Kitaalamu inaelezwa kuwa mmea wenye dawa aina ya Cannabis, inayosababisha aina ua ulevi kwa mtu na zaidi hutumika kwa kuvutwa, ingawa wapo wanaoitumia kwa namna ya kula.

Wapo wanaokuja na hoja zao za kitaalamu, kwamba ina nguvu ya kutibu baadhi ya shida za kiafya.

Serikali duniani zimeharamisha utumiaji bangi, ingawa pia upande wa pili wa shilingi, kuna baadhi ya nchi chache zimehalalisha kuwa dawa za kiafya, bado kuna uthibitisho wa kiafya na mazoea, kuwapo madhara makubwa katika stahimii ya busara ya ubongo.

Hivi sasa katika jamii, kuna kilio cha vijana wengi kulalamika kwamba, wanajihusisha na utumiaji dawa za kulevya ikiwamo bangi, bila ya kujua kuwa kwamba mmea huo wenye majina mengi, unaweza kuathiri afya zao na hata mfumo mzima wa maisha yao.

Katika jamii, kila mtu anaitafsiri bangi kwa aina yake, kulingana na eneo husika, wakiyabatiza majina luluki. Wapo wanaoita 'ganja' wengine msuba, ndumu, marijuana na majina mengine mengi. Bado haifuti ukweli kuwa hiyo ni bangi.

Kuna vijana wanaofanya bangi kuwa sehemu yao ya maisha, kiasi kwamba bila ya kutumia, hawawezi kufanya kitu. Wanalazimika kuitumia kila mara kupitia madai wanapotumia, ndio wanachangamka.

Serikali inawategemea vijana hao katika kulijenga taifa la kesho, hivyo wanatakiwa kuwa kwenye utimamu wa akili na fikra za utambuzi wa mambo, kwa kutumia elimu waliyonayo ili kuzitatua changamoto zinazolikabili taifa lao.

Kumekuwapo ongezeko la vijana wanaovuta bangi katika jamii. Ni jambo linalosikitisha, jinsi vijana hao wanavojivuna wakisema 'bangi ni starehe' kama zilivyo nyingine, huku kukiwapo idadi kubwa ya wasichana kwa sasa nao waejiunga katika starehe hiyo.

Hapo wanaingia wanafunzi katika orodha hiyo. Baadhi yao ni wanavyuo ambao baada ya masomo wanatawanyika katika maneo mbalimbali kuwa ni wataalamu katika jamii. Wameifanya bangi ni biashara vyuoni, kutokana na kuwapo watumiaji wanaohesabika, Ni balaa!

Kwa mujibu wa wataalam na watafiti mbalimbali wa dawa za kulevya, matumizi ya bangi yanaweza kusababisha mvutaji apate matatizo ya akili, huku wakipinga kwa nguvu zote matumizi hayo.

Jijini London nchini Uingereza na Amsterdam Uholanzi, kunasadikiwa bangi zinazouzwa ni zenye ukali ambazo mtu anazitumia, madhara yake ni ya kiwango cha juu zaidi.

Kwa maana hiyo, serikali kama ilivyoanza miaka mingi inatakiwa kuongeza nguvu katika kupiga vita matumizi ya bangi, hususani katika vyuo mbalimbali chini, ambako vijana wengi wanaandaliwa kwa matumizi ya baadaye kitaifa.

AFYA

# Mtafiti Taasisi Ifakara afukua mazito ya kichaa cha mbwa

## • Aorodhesha dalili, madhara • Serengeti kinara wa ugonjwa • Si madaktari wote wanaijua



Wanakijiji wakiwapeleka mbwa wao kupatiwa chanjo, wilayani ya Serengeti. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**.

**Na Beatrice Philemon**

UKIZUNGUMZIA ugonjwa wa 'kichaa cha mbwa' siyo kila mtu anayejua vyema. Hao ni pamoja na watumishi wa afya nchini, baadhi hawaufahamu vizuri, kwa sababu ni ugonjwa usiopewa kipaumbele na kila mtu.

Aidha, wengi hawaripoti kuhusu ugonjwa huo kwa sababu hawazifahamu vyema dalili zake .

Hadi sasa tatizo la ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni kubwa ila kuna changamoto ya kupata takwimu kwa sababu watu hawaripoti ugonjwa huu na ukubwa wa tatizo mara nyingi unaangaliwa katika nyanja tofauti tofauti kwa mfano mifugo inapokufa, nguvu kazi inapungua na pia kutumia resources nyingi sana

Akizungumza na Nipashe, Mtafiti wa magonjwa ya binadamu hasa magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu katika Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) Joel Changalucha anasema kuwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni tafsiri pana, unasababishwa na kirusi kimoja kinachoitwa 'Rabies Virus'

Lakini siyo mbwa tu, ni ugonjwa ambao unaweza kusababishwa na mnyama yeyote anayenyonyesha kama vile paka, mbweha, mbuzi, samba, fisi, ila ugonjwa huu umekuwa maarufu sana kwa sababu mnyama anayeambukizwa zaidi ni mbwa kwa sababu mbwa anang'ata na anaambukiza zaidi kuliko wanyama wengi zaidi.

> "Kwa wastani, maeneo ambayo yana mbwa wengi kwa wastani wa watu 75 kwa kila 100,000 wanaong'atwa na mbwa wanaohisiwa kuwa na kichaa cha mbwa.

### INAVYOAMBUKIZWA

"Mbwa akikung'ata anakuwa na wadudu aina ya Rabies virus ambao wanakaa kwenye mate yake, lakini siyo kila mbwa wote wana kichaa cha mbwa, wengine wanang'ata kwa sababu unakuwa umemchokoza au umechukua watoto wake," anasema

Changulacha anasema, mbwa akishakuwa na kichaa, wadudu wanaenda kwenye mate yake, anapong'ata kwenye jeraha, anaacha mate yanayoambatana na kirusi chenye ugonjwa wa virusi vya kichaa cha mbwa.

"Unapong'atwa na mbwa usipoosha lile jeraha kwa maji mengi na sabuni, kwa hiyo wale wadudu wanazaliana kwenye eneo la jeraha baadae wataingia mwilini kupitia mishipa ya fahamu mpaka kwenye ubongo na inategemea umbali kutoka jeraha lilipo hadi kwenye ubongo na wanasafiri taratibu," anaeleza Changulacha.

Pili, inaelewa kutegemea uwezo wa mtu wa kuhimili au kupambana na magonjwa na idadi ya virusi ambao wameingia kwenye jeraha.

Ili dalili za ugonjwa wa kichaa cha mbwa kuanza kujitokeza kwa mtu aliyeng'atwa na mbwa, safari yao kwa wastani ina chukua miezi 2-3 au hata mwaka mmoja kwa sababu kibailojia wadudu hawa wanatembea milimita tano hadi 100 kwa siku.

### DALILI ZAKE

Changulacha anasema, ni ngumu kumfahamu mtu mgonjwa wa kichaa cha mbwa, kwa sababu dalili zinazojitokeza, zipo sawa sawa na mwenye magonjwa mengine ya kawaida, yaliyozoeleka hospitalini kama malaria na uti wa mgongo, yanayoshambulia mishipa ya fahamu.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limeweka vigezo vya kitabibu vya kumfahamu mgonjwa mwenye kichaa cha mbwa .

Anasema kigezo cha kwanza ni kuchanganyikiwa, kuwa na maumivu ya kichwa, homa, kujikuna mahali alipong'atwa na mbwa, anaogopa mwanga na maji, na hawezi kunywa maji, huku anakuwa amechanganyikiwa na kutokwa na mate mengi mdomoni, kupooza na hatimaye kifo.

Ili kumthibitisha mgonjwa wa kichaa cha mbwa, WHO imeweka vigezo vitatu. Cha kwanza, ni kwamba mtu anathibitishwa kwa kuhisiwa, yaani kama dalili zote kama vile kuchanganyikiwa, kuwa na maumivu ya kichwa, homa, kujikuna alipong'atwa na kuogopa mwanga na maji, huku anashindwa kunywa maji, kuchanganyikiwa na kutokwa na mate mengi mdomoni, kupooza zimeonekana au ndugu kazielezea.

Pili, ni pale dalili zote zilizoajwa zimeonekana au historia ya mtu kung'atwa na mbwa na tatu, ni uthibitisho ya kuwepo historia ya kung'atwa na vipimo vya maabara kuthibitisha ugonjwa huo.

### HALI NCHINI

Akielezea hali ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa hapa nchini, anasema, kwanza anakiri changamoto ya takwimu inayoelezea ukubwa wa tatizo, pia namna ugonjwa ulivyosambaa hapa nchini.

"Sisi kama IHI(Ifakara) tunachoweza kusema kulingana na maeneo ambayo tumefanya utafiti, ni kwamba maeneo yote yenye mbwa wengi nchini, matukio ya kichaa cha mbwa ni mengi.

"Na takwimu tulizokusanya mika zaidi ya 10, sehemu tofauti hapa nchini, inaonyesha kuwa idadi ya watu wanaong'atwa na mbwa ambao tunahisi wana kichaa ni wengi kwenye maeneo yenye mbwa wengi," anaeleza Mtafiti Changulacha.

Anayataja maeneo walikofanya utafiti kwa muda mrefu, ni Wilaya za Serengeti, Ngorongoro, Ulanga, Kilombero na Morogoro, pia wilaya zote za mkoa wa Mtwara na Lindi, pamoja na Pemba.

Hayo yanatajwa kuwa sehemu walizojikita zaidi kufanya utafiti na wamegundua sehemu nyingi zenye umiliki mkubwa wa mbwa, hasa wilaya Serengeti, matukio ya kung'atwa na mbwa ni mengi na wanahisiwa kuwa na kichaa cha mbwa.

### UNAMJUAJE MGONJWA?

Changulacha anasema, kwanza kabisa utamuona mbwa au mnyama anabadilika mwonekano na tabia, anaweza kuwa mkali sana, au mpole kupita kuliko alivyozoeleka.

Vilevile, mnyama wa porini hatokuwa na hofu ya kawaida ya binadamu, ilhali katika uhalisia wanyama wengi wa porini wana hofu ya binadamu.

Pia, mbwa au mnyama wa porini atashindwa kula chakula, atakwepa maji au atashindwa kutembea kwa kawaida, anaweza kupooza mwili, kuanzia miguu ya nyuma, yaani miguu ya nyuma inaishiwa nguvu na pia mbwa au mnyama wa porini atakuwa na mate mengi, anadondosha mate mengi.

Wanyama wengine waliozoea kuonekana usiku, wanaanza kuonekana mchana, ni kwa sababu wamechanganyikiwa baada ya kupata ugonjwa huu.

### KUPAMBANA NAO

Mtafiti huyo anasema, ili kupambana na ugonjwa, kwanza binadamu aking'atwa na mbwa anaye-

AFYA

# Mtafiti Taasisi Ifakara afukua mazito ya kichaa cha mbwa



Sambo Maganga, kutoka Taasisi ya Afya Ifakara, akishiriki kuelimisha wanafunzi wilayani Bahi, katika Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani.

hisiwa kuwa na kichaa, ni muhimu kuosha jeraha kwa maji mengi na sabuni ili kuondoa au kupunguza virusi vya ugonjwa huu kuendelea kuingia mwilini.

"Kama sehemu uliyopo hakuna maji, jitahidi kutafuta kimiminika chochote au hata soda au dafu uoshe kwenye jeraha hilo, ili kuondoa virusi ambayo vinaweza kuingia mwilini hadi kwenye ubongo," anasema

Baada ya hapo, mgonjwa awaishwe kwenye kituo cha kutoa huduma ya afya, ili kupata chanjo na hakikisha unakamilisha chanjo zote ambazo umeandikiwa.

Kwa upande wa mbwa, pia kuna chanjo zake, mbwa anachanjwa mara moja kwa mwaka kuzuia ugonjwa huo.

Anasema kichaa cha mbwa hakina tiba, dalili zikijitokeza kuna hatari ya kifo, ina kinga tu. Chagucha anaenedelea: "Kulingana na utafiti ambao tumeufanya kwenye mikoa mbalimbali hapa nchini na kwa takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa watu 1500 wanakufa kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa kila mwaka," anasema.

Anaendelea kuwa tatizo la kichaa cha mbwa ni kubwa, ila kuna changamoto ya takwimu, kwa sababu watu hawaripoti ugonjwa na pia ugonjwa huo haufahamiki kwa watu.

Ombi lake kwa umma ni kwamba, wamiliki wa mbwa popote walipo wahakikishe wanawachanja mbwa wao kila mwaka kwa maofisa mifugo na wafanye ufugaji sahihi . Pia, anawasihi watu wafuate taratibu sahihi za ufugaji bora wa mbwa ikiwamo kuwapa chakula safi , maji kuwafungia ndani na kuwafungulia usiku tu ikiwemo kuwapa chanjo.

"Kwa wastani, maeneo ambayo yana mbwa wengi kwa wastani wa watu 75 kwa kila 100,000 wanaong'atwa na mbwa wanaohisiwa kuwa na kichaa cha mbwa," anasema.

Kwa maeneo ambayo hakuna mbwa wengi, kuna wastani wa watu 19 kwa kila 100,000 kwa mwaka, anasema.

Anataja mkakati ni wao taasisi ya Ifakara, ni kupambana na ugonjwa huo na kwa mwaka 2020/2021, wanafanya kazi na serikali kwa karibu sana, kwa sababu ndiye mtendaji wa shughuli zote katika eneo lolote.

" Tunazo kazi nyingi ambazo tunazifanya kama IHI na lengo letu linaendana na lengo la shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la wanyama linalojulikana kama ' World Organization for Animal Health (OIE) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO),"anasema.

Anasema mwaka 2015/2016 mashirika haya yalikuja na Mpango Mkakati wa Zero by 30 kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa kufikia mwaka 2030.

"Kwa hiyo sisi tunaenda kufanya kazi kubwa, tunajaribu kuhakikisha kuwa sekta ya afya na mifugo wanafanya kazi kwa karibu kutokomeza kichaa cha mbwa," anasema.

Anasema, wameamua kufanya hivyo kwa sababu chanzo cha ugonjwa ni kutoka kwa mifugo yaani wanyama kuja kwa binadamu, kwa hiyo kama sekta mbili zitafanya kazi kwa pamoja wataweza kupunguza ugonjwa huu.

"Kama Wizara ya Afya, itatenga fedha kwa ajili ya kutibu binadamu na ikasahau kutibu chanzo cha ugonjwa. Ina maana itakuwa haijafanya kitu kwa sababu binadamu wataendelea kuathirika," anasema

Anasema IHI, inataka kuhakikisha watu hawa wanafanya kazi kwa pamoja, na ili kupunguza tatizo hili, hivi sasa IHI imetengeneza mfumo maalumu unaoitwa ( Integrated Bite Case Management (IBCM) ambao mtu akienda hospitalini ameng'atwa na mbwa, Ofisa afya ataingiza taarifa zake kwenye mfumo huo.

Anasema, baadaye ofisa mifugo wa eneo anakotokea huyo mgonjwa, ataenda katika eneo hilo kuchunguza hali ya kiafya ya mbwa, kama aliyeng'ata ana ugonjwa wa kichaa au la.

Chagulacha anaendelea kuwa, wakishamaliza kufanya uchunguzi, wanapeleka ripoti kwenye kituo cha afya kuonyesha kuwa mbwa huyo ana ugonjwa wa kichaa.

Lengo la mfumo huo, ni kutumia chanjo za binadamu kikamilifu au kwa matumizi sahihi kwa sababu mtu mwingine anaweza kung'atwa na mbwa, kumbe mbwa huyo ana virusi vya ugonjwa wa kichaa, pia kusaidia wananchi wasiingie gharama kununua chanjo bila sababu za msingi.

" Ofisa mifugo akienda katika kijiji, kata, au kitongoji ambacho mbwa amemng'ata mtu, atampima mbwa huyo kuona kama ana kichaa au la na hii inasaidia, Yule mtu aliyeng'atwa kupata chanjo au kuacha kupata chanjo.

"Pia, kumsaidia kupima ili kuepuka kifo ikiwemo kupunguza gharama kwa serikali kununua chanjo na pia kutumia chanjo bila sababu za msingi," anasema



Mtafiti wa Magonjwa ya Binadamu Yanayotoka kwa Wanyama Kwenda kwa Binadamu katika Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), Joel Changalucha.

Mtafiti huyo anasema, wao IHI wanajaribu mbinu mbalimbali za kampeni za kuchanja mbwa zinafikia watu wengi.

"Hadi sasa tunajaribu mifumo itakayowezesha uitikiaji mkubwa wa wafugaji wa mbwa kwenye kampeni za kufuga mbwa ila kuna changamoto nyingi kwenye kampeni za kuchanja mbwa, kwa sababu watu wengi hawaleti mbwa kwenye kampeni na ndiyo maana ugonjwa unaendelea kuwapo," anasema.

Anasema katika zoezi hili wana kampeni ya nyumba kwa nyumba, ngazi ya kata, kitongoji, ngazi ya kijiji kutoa chanjo kwa mbwa.

"Kwenye kuchanja mbwa, kuna maeneo ambayo tunapendekeza , chanjo za mbwa zifanyike nyumba hadi nyumba, kuchanja ngazi ya kitongoji au kijiji na pia kupendekeza njia sahihi za utoaji wa chanjo za mbwa ikiwamo ushauri," anasema.

Mbali na hilo pia wanatafiti njia sahihi za utoaji chanjo za binadamu na wamependekeza sindano zichomwe kwa njia ya ngozi ili kupunguza idadi kubwa ya chanjo inayotumika badala ya njia ya misuli.

"Pendekezo hili lilitolewa mwaka 2018 na mpaka sasa pendekezo hili limeanza kutumika katika baadhi ya maeneo hasa katika Mkoa wa Mtwara, Lindi, Morogoro na Pemba karibu baadhi ya hospital zimeanza kutumia," anasema.

Pia IHI imefundisha zaidi ya watumishi wa afya 300 jinsi ya kutoa hizo chanjo yaani utoaji wa kinga tiba ya kichaa cha mbwa kuanzia mwaka 2010-2015 katika Mkoa wa Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Morogoro na Pemba.

Mbali na hilo pia wanategemea kuchunguza gharama za uendeshaji kampeni za kuchanja mbwa ili kuangalia chanjo katika ngazi ya kitongoji, kaya au kata ipoje?

Lengo kuu ni kujua gharama za uendeshaji ili kupendekeza mabadiliko ya sera lakini pia kusaidia serikali kupanga bajeti zake au mikakati yake kulingana na majibu ya utafiti.

"Sisi tunafanya utafiti tu ila kama serikali itatupatia fungu la kuelimisha jamii juu ya ugongwa wa kichaa cha mbwa, athari zake, jinsi unavyoambukizwa na namna ya kujikinga tunaweza kufanya kazi hiyo," anasema.

**Pia, kumsaidia kupima ili kuepuka kifo ikiwemo kupunguza gharama kwa serikali kununua chanjo na pia kutumia chanjo bila sababu za msingi.**

### WITO

Anaomba mamlaka zinazohusika zizidi kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huu, na pia wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo wakae pamoja kuangalia rasilimali walizonazo wanawezaje kuzitumia kwa pamoja kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Pia kuhakikisha wanatenga bajeti ya kununua vifaa vya kinga ya chanjo za mbwa na binadamu kwa sababu ni rahisi kukinga na wamiliki wote wa mbwa wahakikishe wanachanja mbwa wao kila mwaka kwa maofisa mifugo kwa sababu kichaa cha mbwa kinasababisha kifo.

AFYA

# Kilio cha ubakaji watoto shida nzito ndani ya jamii



Baadhi ya wananchi wa Kata ya Kiroka, baada ya kujadiliana kuhusu masuala ya ubakaji na ulawiti yanayoendelea kwenye jamii. **PICHA: CHRISTINA HAULE.**

**Na Christina Haule,** Morogoro

WADAU wa masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto nchini wanasema, kufanikiwa kukomesha ukatili huo, ni endapo jamii itatumia elimu wanayopewa kila mara na kufikia hatua kuacha mtazamo hasi unaowaumiza watoto.

Ofisa Programu Mwandamizi kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP-Mtandao) Deogratius Temba, anasema kuna wanajamii wanaikimbilia yasiyofaa kama vile ulevi, tamaa na ushirikina, inayoleta athari kwao watoto kuangukia ubakaji na ulawiti.

Anasema, watu wanaona kuwanyanyasa wenzao bila ya sababu ni jambo la kawaida, pasipo kukumbuka kwamba zote zinaleta ongezeko la vitendo vya ukatili wa kijinsia, kwa watoto ikiwamo ubakaji au ulawiti.

Temba anasema mitazamo hasi kwa jamii imekuwa ikisababishwa na mabadiliko ya kitabia na kujikuta wakijiingiza kwenye mambo ya ushirikina, ulevi na tamaa inayochangia ukatili wa kijinsia kwa kasi kubwa kwa watoto kwa sasa.

Aidha, anasema jamii inapaswa kuachana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji huku wakitambua Sheria Maalum ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998 na sheria nyingine ya makosa ya jinai inayomuacha mtu katika kifungo miaka 30 jela.

> **Kutokana na uhalisia huo, wanaendelea kushirikiana na serikali katika halmashauri 22, kubadilisha mitazamo hasi ya jamii, ili kupunguza ukatili kwa watoto.**

### TGNP YAINGILIA

Ofisa Programu huyo wa TGNP, anasema ni adhabu kubwa, lakini kuna sehemu ya jamii bado inaonekana kutoogopa kwa kuendekeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Anasema, kutokana na uhalisia huo, wanaendelea kushirikiana na serikali katika halmashauri 22, kubadilisha mitazamo hasi ya jamii, ili kupunguzao ukatili kwa watoto.

Temba anazitaja halmashauri wanazoshirikiana nazo ni Simanjiro, Mpwapwa, Chamwino, Serengeti, Tarime, Kishapu, Kigoma, Kasulu, Mbeya, Morogoro Vijijini, Ilala, Kinondoni, Ubungo, Temeke, Kisarawe, Kasulu Mji, Same, Muheza, Kilindi, Pangani, Mbarali na Mbozi.

Anasema, huwa wanafanya uhamasishaji kupitia vituo vya taarifa na maarifa wakielimisha jamii iondokane na mitazamo hasi.

Temba anasema sehemu ya Mpangokazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa) wanaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha malengo na viashiria vyake vinatekelezwa ifikapo mwaka 2021 na kuleta matokeo sahihi mwaka 2022, utakapokamilika.

Temba anavitaja viashiria vya Mtakuwwa ni kupunguza mimba za utotoni kutoka asilimia 27 hadi asilimia tano na kupunguza kiwango cha ukeketaji kutoka asilimia 32 hadi 11, pia ndoa za utotoni kutoka asilimia 47 hadi 10.

Anasema, viashiria hivyo vinaweza kuwa njia sahihi ya kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini.

TGNP baada ya kuhakikisha uundwaji kamati za Mtakuwwa, inajipanga kuwajengea uwezo, ili kamati hizo zitekeleze majukumu yake inavyotakiwa, kuanzia ngazi za vijiji, wilaya hadi Taifa.

### MSAADA SHERIA

Akizungumzia usimamizi wa kisheria unaofanywa na wasaidizi wa kisheria kutoka Kituo cha Msaada wa Kisheria mkoani Morogoro (MPLC), Msaidizi wa Kisheria, Joyce Peter, anasema ifike wakati jamii iepuke kuwaweka katika mazingira hatarishi watoto.

Joyce anasema, kumuacha mtoto nje usiku kwenye maeneo kama vilabu vya pombe, ni hatari na mara nyingi wanawashauri wazazi wa mtoto aliyebakwa kutokubali kuyamalizia nyumbani, kwani kufanya ni kuendeleza matendo hayo.

Kwa mujibu wa mwanasheria huyo, wanatumia vifungu mbalimbali vya sheria kuwapa msaada wazazi na walezi wanaofika ofisini kwao, kupata msaada wa kisheria.

Sakina Nyumayo, Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa MPLC, anasema wanakuwa na kesi wanazozitolea ushauri kwa matukio ya ukatili kijinsia, ubakaji na ulawiti.

Kwa mujibu wa Sakina, mwaka 2019 walipokea kesi 32 kwa mwaka 2019 na mwaka 2018, kesi 276, ikiwa tofauti ya kesi 244 pungufu, kiashiria kwamba matukio hayo yamepungua kwa sababu ya juhudi zinazofanywa na mashirika, pia wadau kutoa elimu, ikiwamo kupitia midahalo, redio, televisheni na magazeti.

Anasema, bado kuna wazazi wanaoendelea kuficha mikasa ya ukatili wa kijinsia wanayofanyiwa watoto wao, ikiwamo kubakwa, wakiona ama aibu au kuhofia mwanamume kufungwa, wakati binti yao ameshapewa mimba, wakimtarajia mtu huyo atawapa msaada.

### WAKAZI

Mkazi wa Kata ya Kiroka, Mkoa wa Morogoro, Maria Magari (29), anashauri haja ya serikali kutilia maanani suala la hatua kali, kwa watoto matukio ya ubakaji, ili amri iogope kuendekeza matendo hayo, ikiwamo kwa wazazi wanaokubaliana nje ya sheria

Maria anasema, serikali kwa kutumia sheria zilizopo wawe na ukali, jambo litakalokomesha vitendo hivyo kumalizika kiholela, wahusika sasa wakihofu.

Abeid Kambi (51), mkazi wa Kiroka, anahimiza serikali kutathmini uhalali wa nafasi uwepo wa waganga wa jadi, katika namna wafanyavyo kazi, akirejea mikasa ya watu kufikia hatua ya kuwabaka watoto zao, wazee vikongwe kubaka na kinyume chake .

Kambi anasema, mara nyingi jamii inapoteza amani yake, kisa kikuu ni ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji na kutokana kutimiza masharti wanayopewa na waganga wa jadi, baadhi katika dai la kusaka utajiri.

Anasema, mtoto anayefanyiwa ukatili hata uzoefu unaonyesha anaharibiwa kisaikolojia na kuna wakati juhudi zake za darasani zinafifia.

### TAMWA

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari wanawake Tanzania (Tamwa) Rose Reuben, kwenye Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia mwaka jana, inalinukuu Shirika ka Umoja wa Mataifa la Watoto kwamba wabakaji wengi ni ndugu wa karibu.

Rose anaiomba serikali na wadau wengine wa masuala ya haki za watoto, kuendelea kupaza sauti zao za kuhakikisha ukatili wa kijinsia kwa watoto unapungua na ikiwezekana kumalizika kabisa.

Anahimiza usemi 'Mtoto ni Taifa la Kesho' hivyo anapaswa kulindwa na anasisitiza jamii kutambua kuwa suala la kupinga ukatili wa ubakaji na ulawiti kwa watoto ni jukumu la wote na ifikie mahali kila mmoja awe mlinzi wa mtoto, kwa kutoa taarifa za matukio ya ukatili.



# RC awacharukia matapeli wanaozua migogoro ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JIJI la Mbeya linadaiwa kuwa na ongezeko kubwa la matapeli wanaouza viwanja na nyumba kwa njia zisizo rasmi, hali ambayo inasababisha uwepo wa migogoro mingi inayokwamisha maendeleo ya baadhi ya wananchi.

Hali ya kukithiri kwa migogoro hiyo ya ardhi imemkera Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, ambaye juzi alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, kutumia vyombo vyake vyote vya ulinzi na usalama kuwasaka matapeli hao na kuwafikisha mbele ya sheria.

Chalamila alitoa agizo hilo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Mtaa wa Gombe Kusini ikiwa ni baada ya kutiwa mbaroni kwa Atuganile Kalenge, ambaye anatuhumiwa kuwatapeli baadhi ya wananchi wa mtaa huo.

Alisema mtuhumiwa baada ya kuwatapeli wananchi hao, alikimbilia Ikulu jijini Dar es Salaam ambako alikwenda kumweleza Rais John Magufuli kuwa anatishiwa kuuawa na kwamba hana imani na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya.

"Hili sisi Serikali hatuwezi kulivumilia hata kidogo," alisema Chalamila na kuongeza kuwa baada ya mtu huyo kutoa malalamiko yake Ikulu, Rais Magufuli alimpigia simu na kumuagiza kushughulikia malalamiko hayo, lakini baada ya kufika eneo lwa lengo la kufuatilia malalamiko yake akabaini kuwa mtu huyo huyo ni tapeli.

Alisema aliamuaru atafutwe popote alipo kwa gharama za Serikali na kukamatwa ili ajibu tuhuma hizo na Jeshi la Polisi limeshamkamata.

Baada ya kukamatwa, Chalamila aliamua kumrejesha mtaani hapo na ndipo wakaibuka watu wengine zaidi ya watano ambao pia walikuwa wakimlalamikia kuwa aliwatapeli, huku wakiwataja na watuhumiwa wengine wa utapeli, ambao pia wanadaiwa kuwa ni rafiki zake.

"Hapa nimejiridhisha kuwa mji huu unao matapeli wengi wanaowaibia wananchi kupitia biashara hii ya viwanja, hivyo basi nakuagiza Mkuu wa Wilaya,



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akimsikiliza Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mkoa wa Mbeya, Nelusigwe Kajuni (wa pili kulia), wakati chama hicho kilipokabidhi mifuko 200 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa shule maalumu ya sekondari katika Jiji la Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Shirika lasaidia wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

SHIRIKA la Child Support Tanzania (CST), linalojihusisha na masuala ya elimu jumuishi mkoani Mbeya, limetoa msaada wa Sh. milioni 200 ili kukabiliana na vikwazo mbalimbali vinavyowakumba watoto wenye ulemavu katika Wilaya ya Rungwe.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mradi wa 'Peleka rafiki zangu wote shuleni' uliozinduliwa wilayani Rungwe, Mkurugenzi wa Shirika la Child Support Tanzania, Noela Msuya, alisema mradi huo unalenga kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum kwa kuwapatia vifaa sadizi ikiwamo baiskeli, fimbo pamoja na ukarabati wa shule ili kukidhi mahitaji ya watoto hao.

Msuya alisema mradi utazinufaisha shule tano za msingi ambazo ni Masebe, Magereza, Ibhaga, Katumba II na Nzunda na kwamba utadumu kwa miaka miwili.

"Nia yetu ni kuhakikisha elimu jumuishi inaongeza ufaulu kwa watoto wenye ulemavu kama ilivyo kwa wengine kwa kujengewa miundombinu rafiki sambamba na kuwajengea uwezo walimu mbinu mbalimbali za kufundishia pamoja na wanafunzi wasio na ulemavu kuwaripoti wenzao walioficha nyumbani ili wasipate elimu," alisema Msuya.

Aliongeza wanatarajia kuwapatia maarifa walimu 20 mahususi kwa ajili ya kuwahudumia watoto 200 wenye ulemavu ambao wako nyumbani, vikundi vya wazazi na walezi 125, viongozi wa serikali za mitaa 50 pamoja na klabu za haki za watoto 150.

Akizungumza kwa niaba Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Katibu Tawala wa Wilaya, Mnkondo Bendera, alisema watafanya kikao maalum ili kujadiliana namna fedha hizo zitatumika kumaliza vikwazo vilivyopo kwenye elimu jumuishi.

Alisema watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwemo miundombinu ya majengo, vifaa vya kujifunzia na kwamba Halmashauri kila mwaka wanatenga asilimia mbili ili kulisaidia kundi hilo.

Aliongeza Sh. milioni 200 ambazo zimetolewa na Shirika la Child Support Tanzania CST, zitaongeza nguvu ya kukabiliana na vikwazo mbalimbali vinavyokabili mfumo wa elimu jumuishi.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wilayani Rungwe, Emu Mwasofu, alidai bado kuna tatizo kubwa kwenye jamii kuwaficha watoto wenye ulemavu hali inayosababisha wakose haki ya elimu.

Alisema jukumu la kuwaibua watoto wenye ulemavu ambao wamefikia umri wa kwenda shule linatakiwa kufanywa kwa ushirikiano badala ya kuliachia Shirika la CST pekee.

Diwani wa Kawetele, Anyimike Mwasakilali, aliomba Shirika kuzifikia shule zote za msingi wilayani Rungwe ili kumaliza kabisa matatizo yanayowasibu watoto wenye ulemavu kupitia mfumo wa elimu jumuishi.

## Rungwe walia kukosa X-ray

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wa Wilaya ya Rungwe, wanalalamikia kukosekana kwa kipimo cha mashine ya X-ray kwa wiki mbili katika Hospitali ya wilaya hiyo Makandana, hali ambayo inawalazimu kutumia gharama kubwa kwenda katika Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya.

Wakizungumza na Nipashe juzi wananchi hao walisema ukosefu wa huduma hiyo ni tatizo kubwa kwa wagonjwa wao wa kawaida na wa dharula ambao wanapata ajali.

Tumaini Nyerere, alisema huduma ya X -ray ni muhimu, hivyo wanaiomba serikali kuifanyia matengenezo ya haraka ili kuwezesha wananchi kupata huduma hiyo katika hospitali hiyo.

Alisema ikitokea mtu ana mgonjwa anayetakiwa kupimwa kipimo hicho ni lazima ampeleke Mbeya Mjini ama katika Hospitali ya Misheni ya Igongwe.

"Ni jambo la kusikitisha kwa sababu mashine ya X-ray kutofanya kazi ni hatari, kuna wagongwa wa dharula ambao wanaweza kupoteza maisha kutokana na kukosa huduma hiyo, kutoka hapa mpaka Mbeya ni mbali, hivyo gharama zinaongezeka sana," alisema Tumaini .

Antony Mwaisaka, alisema licha ya kukosekana kwa huduma hiyo, pia wauguzi katika hospitali hiyo hawafanyi kazi kwa wito jambo linalochangia huduma kudorola siku hadi siku na kuwapo kwa msongamano mkubwa wa wagonjwa.

Alisema hivi karibuni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipofanya ziara katika Hospitali hiyo alikuta huduma ni mbovu na akawakemea lakini bado mabadiliko ni madogo.

Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. John Mrina, alikiri kuwapo kwa tatizo la mashine ya x-ray, na kwamba sababu za kuharibika ni tatizo la umeme kukatika mara mara.

"Mashine ilikuwa ikifanya kazi, lakini kutokana na kukatwa kwa umeme mara kwa mara ndio imepelekea kifaa kimojawapo kimeungua, hivyo baada ya siku mbili itakuwa imetengamaa... kuna fundi anakuja kutoka jijini Dar es salaam," alisema Dk. Mrina.





# Watakiwa kuhimiza amani uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa jumuiya ya maridhiano mkoani Dodoma, wametakiwa kuhamasisha wananchi kulinda amani kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Askofu Evance Chande, alipokuwa akizungumza na viongozi wa Wilaya ya Kongwa kwenye ziara yake ya kuangalia uhai wa jumuiya hiyo.

Alisema viongozi wa dini wana wajibu mkubwa wa kutoa elimu kwa waumini na kwa viongozi wa siasa ili amani iliyopo idumu kwa maslahi ya Watanzania wote.

"Tunapokwenda kwenye uchaguzi mwaka huu viongozi wa jumuiya hii muwe mabalozi wa kulinda amani ili ufanyike kwa uhuru na amani kwa Watanzania wote," alisema.

Kiongozi huyo, alisema amani isipodumishwa gharama ya kuirudisha itakuwa ni kubwa hivyo ni muhimu kuitunza.

"Nafasi yetu ni kuelimisha wale wote watakaojitokeza kugombea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu ili walinde amani yetu," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mshauri Mkuu wa jumuiya hiyo, Mchungaji John Mariga, aliwataka viongozi hao kutonyoosheana vidole kutokana na tofauti zao za madhehebu, bali wawe kitu kimoja katika kulinda na kudumisha amani.

"Fanyeni kazi hii kwa umoja na mshikamo pamoja na viongozi wa serikali na pia mjiepushe na matumizi ya fedha kwa waumini ili muaminiwe kwenye utendaji wenu," alisema.

Naye, Katibu wa jumuiya hiyo, Bakari Bakari, aliwataka viongozi kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa ni kioo cha jamii.

Awali, akisoma taarifa ya jumuiya hiyo wilaya ya Kongwa, Katibu wa Wilaya, Salumu Mkole, aliomba jumuiya hiyo kutambulishwa kwa viongozi wa serikali na siasa kutokana na kutotambuliwa.

"Tumekuwa na shida kubwa kwetu hapa, baadhi ya viongozi wa siasa na dini hawatutambui hivyo kusababisha kuifanya kazi hii kwa ugumu mno," alisema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Evance Chande akizungumza na viongozi wa jumuiya hiyo, katika kikao cha kutathmini utendaji kazi kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kongwa jana. Kushoto ni Mshauri Mkuu wa jumuiya hiyo, Mchungaji John Maliga na Katibu wa Jumuiya, Ustadhi Shabani Shabani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Sera mpya ya kilimo mbioni kuinuliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali inatarajia kuja na sera ya kilimo ambayo inalenga kuinua sekta hiyo.

Akizungumza katika Kongamano la sita la wadau wa sera za kilimo, mifugo na uvuvi, Bashe alisema sera hiyo itakuwa mkombozi mkubwa kwa mkulima.

"Kilimo kimekuwa na matatizo mengi na sasa unakuja muarobaini wa kupunguza ili kundi kubwa la watu wanaotegemea kilimo kiwainue... hii ni sekta iliyoajiri wananchi wengi na ukuaji wa sekta ya kilimo ni asilimia 5.3, ni muhimu kuangalia kiasi gani kimewekezwa kwenye bajeti na tunakosea wapi," alisema.

Hata hivyo, alisema wanataka vyama vya ushirika vifanye kazi na kutoa matokeo yaliyokusudiwa.

Aidha, Bashe alisema serikali iko tayari kuendeleza sekta binafsi kwa kuwa ndiyo inayochangia pato la Taifa kwa asilimia kubwa katika sekta mbalimbali ikiwamo ya kilimo. Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo Tanzania, Jitu Soni, alisema Tanzania imekuwa ikitumia mbolea kwa kiwango kidogo sana ikilinganishwa na nchi ya Kenya.

Alieleza kuwa kiasi ya kilo 18 kwa hekta kimekuwa kikitumika kwa Tanzania huku Kenya ni wastani wa kilo 50 kwa hekta.

Akizungumzia utafiti uliofanyika kwenye mikoa tisa nchini kwa misimu mitatu ya kilimo, Soni alisema ilibainika kuwa usambazaji wa mbolea kutoka Dar es Salaam kwenda kwa wakulima mikoani, bei elekezi ilishindwa kufuatwa kutokana na kero za usafiri. "Baadhi ya maeneo mbolea ilikuwa haitoshi pia, mbolea iliyokuwa ikiagizwa ilikuwa ikienda nchi za jirani, jambo la msingi ni kuhimiza uzalishaji wa mbolea hapa nchini," alisema.

Mwenyekiti wa timu ya wachambuzi wa sera na Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la wadau wa kilimo wasio wa kiserikali (ANSAF), Audax Rukonge, alisema bado kiwango cha mbolea kinachotumika kwenye mashamba ni kidogo.

# Wakuu wa polisi nchi 14 kukutana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa vikao vya kamati tendaji za Shirikisho la Wakuu wa Polisi wa nchi za Mashariki mwa Afrika, unatarajiwa kuanza leo jiji la Dar es Salaam ambao unalenga kujadili namna ya kupambana na uhalifu unaovuka mipaka ndani na nje ya nchi hizo.

Mkutano huo utahusisha kamati ya Wakurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mafunzo, Sheria, Jinsia pamoja na kamati ya kuzuia na kupambana na vitendo vya kigaidi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, alisema mkutano huo utaanza Februari 20 hadi 21, mwaka huu na utafunguliwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Simon Sirro, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Shirikisho hilo.

Alitaja nchi zitakazoshiriki katika mkutano huo ni Burundi, Comoro, Djbouti, Kongo (DRC), Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Seychells, Somalia,Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Tanzania.

Alieleza kuwa mbali na kujadili namna ya kupambana na uhalifu unaovuka mipaka, pia utapitia utekelezaji wa maazimio ya mkutano mkuu uliofanyika Septemba mwaka jana jijini Arusha.

"Aidha, utatanguliwa na warsha ambayo itahudhuriwa na wataalam wa kuzuia na kupambana na ugaidi katika nchi hizo 14," alisema.

Alibainisha kuwa mkutano unatarajiwa kutoka na mapendekezo ya namna ya kupambana na uhalifu unaovuka mipaka ikiwamo uhamiaji haramu na vitendo vya kigaidi.

Alisema lengo ni kuweka mikakati ya pamoja ya kudhibiti uhalifu wa aina hiyo.

Akizungumzia kuhusu hali ya ulinzi na usalama nchini, Misime alisema hali ni shwari na yale matukio machache yanayojitokeza yanaendelea kudhibitiwa.



# Dk. Shein awataka watendaji Ardhi kuwa waadilifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kuendeleza uzalendo na uadilifu katika kazi.

Akizungumza jana Ikulu Zanzibar wakati alipokutana na uongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati wakati ilipowasilisha utekelezaji wa Mpango Kazi kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2019/2020, aliwataka viongozi hao kuendeleza kushirikiana na kuendeleza kasi ya kuwa wazalendo kwa kupenda vyao na kuithamini nchi yao na kuwa waadilifu katika kazi.

Dk. Shein aliutaka uongozi huo kufuata taratibu na sheria katika kufanya uamuzi ili kuepuka sintofahamu kwa wananchi na kuwataka kutumia busara katika utendaji kazi wanapoitumikia jamii.

Alihimiza umuhimu wa taarifa kwa viongozi wa mamlaka ya juu wanapotekeleza majukumu yao huku akiwataka viongozi hao pamoja na watendaji wa wizara hiyo kuongeza kasi ya utendaji wa kazi zao ili kufikia malengo waliyokusudia.

Dk. Shein pia aliitaka Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kuongeza kasi katika utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu uingiaji wa vyombo vya moto kwa kushirikiana na taasisi nyingine ili zoezi hilo liende vyema. Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), imetakiwa ndani ya mwezi mmoja kuweka huduma ya umeme unaotumia nguvu za jua katika kisima kimoja wapo kwenye visima vinavyosimamiwa na mamlaka hiyo.

Naye Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, alisema wizara yake inatekeleza malengo na mikakati ya serikali ya kuhakikisha wananchi wa visiwa vya Zanzibar wanapata huduma stahiki. Alizitaja huduma hizo kuwa ni pamoja na maji, nishati ya uhakika iliyo salama na endelevu, makazi bora na matumizi mazuri ya ardhi yenye kukidhi mahitaji ya wananchi na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii.

Alisema wizara yake kupitia Mamlaka ya Maji (ZAWA) imeendelea kusimamia miradi na programu za uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini na usambazaji wa maji vijijini.

Alisema katika utekelezaji wa programu hiyo, Mamlaka ya Maji kupitia mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi (ADF12), imekamilisha kazi ya utekelezaji wa mradi kwa uchimbaji wa visima vipya sita vyenye uwezo wa wastani wa lita 150,000 kwa saa kwa kila kisima.

Ukarabati wa visima vikongwe 23, ujenzi wa matangi mawili yenye ujazo wa lita milioni mbili Saateni na milioni moja la Mnara wa Mbao pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 75.7. Alisema wizara hiyo kupitia Shirika la Umeme katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, imefanikiwa kutekeleza azma ya serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya umeme katika maeneo yao kwa kufikisha umeme katika vijiji 26 (Unguja 16 na Pemba 10) na jumla ya Sh. bilioni 1.96 zimetumika.




Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadil Abdullatif (kushoto), akizungumza na Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaonya wanaosambaza picha ya mtoto mgonjwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI imewaonya watu wanaosambaza picha ya mtoto anayesumbuliwa na kansa ya ngozi kwa nia ya kutafuta michango ya wafadhili kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Kadhalika Wizara ya Afya Zanzibar imesema kuwa inaendelea kutekeleza sera kwa kuhakikisha wananchi wanapatiwa matibabu bure pamoja na kuwasafirisha wagonjwa nje ya nchi.

Waziri wa wizara hiyo, Hamad Rashid Mohamed aliyasema hayo juzi huko Hospitali ya Rufani Mnazi mmoja katika wodi ya wagonjwa wa ngozi.

“Kuisambaza picha ya mgonjwa katika mitandao ya kijamii ni kosa la kumdhalilisha pia kwenda kinyume na Sera ya Serikali,” alisema Waziri Hamad. Alisema serikali inatumia pesa nyingi kununua vifaa tiba ili kuhakikisha wananchi wanapatiwa matibabu ya uhakika na wale wanaohitaji kusafirishwa nje hupelekwa kwa matibabu zaidi.

Naye Daktari wa magonjwa ya ngozi katika Hospitali ya Mnazimmoja, Hafidh Sheha Said, amekiri kumpokea mtoto Saidi Ali Ayoub, mwenye umri wa miaka mitatu kutoka Micheweni Pemba mwishoni mwa mwaka jana ambaye anasumbuliwa na ugonjwa wa ngozi ambao hauwezi kupokea mionzi ya jua .

Alisema mtoto huyo baada ya kugundulika ana saratani ya ngozi katika kichwa chake, alisafirishwa na kupelekwa Hospitali ya Muhimbili kwa kupatiwa matibabu zaidi.

Dk. Said alisema mtoto huyo alirejea kutoka Muhimbili baada ya wazazi wake kuona tiba anayopatiwa haimpi unafuu bali ni kumuongezea majeraha. Alifafanua kuwa ngozi ya watoto kama hao ambao wanaitwa watoto wa usiku, wakipata mionzi ya jua hupata saratani ya ngozi hivyo hupatiwa mafuta maalum ya kupaka, miwani pamoja na kofia.

Baba wa mtoto huyo, Ali Ayoub Hamad, aliiomba serikali kumsaidia kumpatia matibabu mtoto wake ili aweze kupona.

“Nimemzaa mtoto wangu akiwa mzima kufika miezi saba tu akaanza kutoka vidoti vyeusi, vikasambaa kichwani na kutoka vidonda,” alisema.

## Hospitali za wilaya kufanyiwa ukarabati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema hospitali za wilaya ambazo zipo chini ya halmashauri zitafanyiwa ukarabati mkubwa ili kutoa huduma za afya kwa ufanisi.

Naibu Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya ukarabati wa baadhi ya hospitali za wilaya ambazo zipo chini ya halmashauri za wilaya.

Alisema baadhi ya vituo vya afya ambavyo vipo katika mpango wa ugatuzi kwenda serikali za halmashauri vimefanyiwa matengenezo makubwa kwa ajili ya kutoa huduma za kinamama na watoto.

Alivitaja vituo vilivyofanyiwa ukarabati ili kutoa huduma hizo ni Mwembe Makumbi, Mpendae Chumbuni, Mwera na Kiboje Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema Wizara ya Afya kwa ushirikiano na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa imechukua uamuzi huo ili kupunguza msongamano wa kinamama wengi kupata huduma zao katika Hospitali ya Mnazimoja na Mwembeladu, Unguja.

“Tutazifanyia ukarabati hospitali za wilaya ambazo zipo katika mpango wa ugatuzi kwaajili ya kutoa huduma za wajawazito na watoto kwa lengo la kupunguza msongamano,” alisema.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa, Haji Omar Kheir, alisema hospitali zote za wilaya zipo chini ya mpango wa ugatuzi wa halmashauri kwa ajili ya kutoa huduma za sekta ya afya.

Alisema kwa ushirikiano mzuri na Wizara ya Afya, wamefanikiwa kukarabati baadhi ya hospitali za vijijini ambazo hutoa huduma za wajawazito na watoto.

“Uhusiano wetu mzuri kati ya Wizara ya Afya na Serikali za Mitaa sasa umewezesha ukarabati zaidi ya vituo vya afya tisa na kuwa na hadhi ya kuwawezesha wajawazito kupata huduma za kujifungua,” alisema.

# Tanroads yataka matumizi sahihi ya madaraja

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WANANCHI mkoani Kagera wametakiwa kutambua matumizi sahihi ya madaraja ambayo ni mapitio ya maji na kuwa waangalifu wa shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.

Hayo yamesemwa na Meneja Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) mkoani Kagera, Andrea Kassamwa, alipozungumza na Nipashe kuhusu matengenezo ambayo hufanyika kila mwaka hasa katika kuelekea msimu wa mvua za masika.

Kassamwa alisema matengenezo ya mara kwa mara yamekuwa yakiingiza serikalini katika gharama kwani sababu kubwa ni wananchi kukosa elimu, uangalifu na uthamini wa miundombinu ya barabara.

"Kila mwaka tuna bajeti ya matengenezo ya makalavati, kwa mwaka huu wa fedha 2019/20 bado tunaendelea kurekebisha kufanya matengenezo yanayo kuwa yamesababishwa na wananchi na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha kwa mkoa wetu," alisema.

Alisema kazi zinazofanyika ni matengenezo ya kusafisha, kuzibua na kurudia sehemu iliyoharibiwa na kwamba madaraja 261 kwa barabara kuu yanaendelea kutengenezwa ambapo madaraja ya kawaida kwa barabara za mkoa ni 151.

"Tuna jumla ya madaraja 261kwa barabara kuu zote zilizo mkoani hapa na tuna madaraja 151. Yale ya kawaida kwa maana yaliyopo mkoani kuanzia mjini Bukoba ambako tunaohusika ni Tanroads pekee," alisema Kasamwa.

# Viongozi Amcos wafunguka kupotea fedha za wakulima

**Na Happy Severine,** SIMIYU

VIONGOZI wa Vyama vya Ushirika Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, wametaja sababu za kuonekana wametumia vibaya fedha za wakulima wanapofanyiwa ukaguzi au kulalamikiwa na wakulima.

Walisema kuwa sababu kubwa ya wao kuingia katika tuhuma hizo, ni kukosa mafunzo yanayohusiana na matumizi ya fedha, jinsi ya kuandaa taarifa za fedha, mapato na matumizi.

Walibainisha hayo, baada ya kuwapo kwa tuhuma nyingi dhidi ya viongozi hao, huku baadhi yao wakishtakiwa na kufungwa, na wengine kuuza mali zao ili warejeshe fedha walizotumia vibaya. Walisema hayo wakati wa mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Simiyu (SIMCU), yaliyolenga kuwajengea uwezo wa jinsi gani ya kuandaa na kutoa taarifa za fedha.

Mafunzo hayo ambayo yaliwashirikisha wahasibu kutoka Amcos 73 wilayani humo, yalilenga pia kuwapatia elimu ya utunzaji wa vitabu vyao vya uhasibu, kuandika mahesabu vizuri, kufunga vitabu na kutunza kumbukumbu zao ili kuepuka kupata hati chafu.

Walisema kuwa wakati mwingine hesabu zao zinakuwa vizuri, lakini jinsi ya kuzipanga na kuzitoa taarifa ndiyo imekuwa changamoto kubwa kwao na kujikuta wameingia kwenye tuhuma hizo.

"Wahasibu wengi wanaofanya kazi kwenye vyama hivi hawana taaluma yoyote ya uhasibu wala mafunzo hatuna, ndiyo maana kila siku tunatuhumiwa, wengine hatujui kufunga na kufungua vitabu vya hesabu," alisema John Kaboye.

" Lakini hata kuandaa taarifa za fedha nalo ni tatizo, wakija wakaguzi wanakuta hesabu haiko vizuri... tatizo ni jinsi gani ya kuandaa hizo taarifa, kuziwasilisha, lakini hata kutunza kumbukumbu za uhasibu," alisema Maria John.

Viongozi hao wameishukuru SIMCU kwa kuleta mafunzo hayo ambayo walisema yatawaondoa kwenye misukosuko ambayo wamekuwa yakiipata kila mara kwenye malipo ya wakulima na matumizi ya vyama vyao.

Mrajisi msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa mkoa huo, Ibrahimu Kadudu, alisema kuwa ofisi yake kwa kushirikiana na SIMCU wamelenga kutoka mafunzo kwa wahasibu wote mkoa mzima 336.

Awali akifungua mafunzo hayo Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Titus Kamani, aliwataka viongozi wa vyama hivyo kufanya kazi kwa weledi na ushirikiano ili kuwakomboa wakulima nchini.



Mmoja wa washiriki wa kongamano linalohusu jinsi ya kukabiliana na mgogoro wa madeni mapya kwa nchi za Afrika, Dk. Blandina Kilama, akichangia mada kwenye kongamanmo hilo lililofanyika katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), jijini Dra es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wilaya ya Kilolo wafagilia TRA kufungua ofisi

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa wamefurahia hatua ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufungua ofisi wilayani humo na kusema kuwa kutaongeza tija katika ukusanyaji mapato ya serikali.

Wamesema hatua hiyo kumewasaidia kuwapunguzia umbali wa kilometa 60 walizokuwa wanatembea kwenda Iringa mjini kufuata huduma ya TRA.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea mkoani humo, wananchi hao walisema kuwa, awali walikuwa wakisafiri umbali mrefu kwenda Iringa mjini kufuata huduma za TRA na kusababisha kutumia muda mwingi tofauti na ilivyo hivi sasa.

Mmoja wa wafanyabiashara wa vipodozi wilayani humo, Prosper Mwinu, alisema ufunguzi wa ofisi hiyo pia utawaondolea gharama walizokuwa wakizitumia kufuata huduma za TRA Iringa mjini.

"Tunaishukuru Mamlaka ya Mapato kutusogezea huduma karibu kwa kutufungulia ofisi hapa Kilolo maana tulikuwa tunatumia gharama za kusafiri kwenda Iringa mjini kuifuata huduma na wakati mwingine tulikuwa tunaingia gharama za kulala huko ikitokea tumeshindwa kupata huduma zote kwa siku moja," alisema Mwinu.

Grace Barnaba, mfanyabiashara wa duka la pembejeo alisema wananchi wanapokuwa wamesogezewa huduma karibu wanakosa sababu ya kutokulipa kodi kwa wakati kwani hawakutani na foleni na hupata huduma hizo kwa haraka.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Asiah Abdallah, alisema ufunguzi wa ofisi ya TRA wilayani Kilolo umewapa faraja wananchi kwa sababu awali walikuwa wakitembea umbali mrefu zaidi ya kilomita 60 kwenda kutafuta huduma za kulipa kodi.

"Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba, tumepiga hatua kubwa sana kuwapo kwa ofisi ya mapato katika wilaya yetu ya Kilolo na hivyo tunategemea uchumi wa wilaya yetu utaongezeka kutokana na kwamba wananchi sasa watakuwa wanalipa mapato katika njia ambayo ni rafiki na rahisi," alisema Abdallah.

Kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea mkoani Iringa ilianza Februari 17, mwaka huu na inatarajia kumalizika Februari 22, mwaka huu ikiwa na lengo la kuwaelimisha wafanyabiashara na wananchi masuala mbalimbali yanayohusu kodi.

HABARI KIMATAIFA

## Ndege za boeing zakutwa uchafu kwenye matenki

**WASHINGTON,** Marekani

SHIRIKA la Boeing linakumbwa na hatari ya kukabiliwa tena na suala la usalama katika ndege zake baada ya uchafu kupatikana kwenye tengi za mafuta katika baadhi ya ndege ambazo zilikuwa zinasubiri kuwasilishwa kwa wanunuzi.

Msimaizi wa ndege aina ya Boeing 737, aliwaambia wafanyakazi wake kwamba ugunduzi huo ni jambo lisilokubalika.

Msemaji wa shirika hilo alisema kwamba kampuni hiyo haikugundua tatizo hilo na kusababisha ndege hizo kuchelewa zaidi kuanza tena huduma zake. Jambo hilo limetokea wakati ambapo ndege aina ya 737 Max bado hazijaidhinishwa kurejea kutoa huduma baada ya kusababisha ajali mbili mbaya ambapo abiria walipoteza maisha.

Shirika hilo la Marekani lilisema kwamba limegundua uchafu ulioachwa ndani ya matenki ya fueli kwa ndege kadhaa za 737 Max ambazo hazijawasilishwa kwa wateja.

Uchafu ulioktwa ni kama vile vifaa vya metali na vingine vilivyoachwa na wafanyakazi wakati inaunganishwa. **BBC**

## Wafanyakazi wasio na ujuzi marufuku kuingia Uingereza

**LONDON,** Uingereza

UINGEREZA inatarajia kuanzisha mfumo mpya wa uhamiaji bada ya kujitoa Umoja wa Ulaya (EU), ikitoa kipaumbele kwa wafanyakazi wenye ujuzi duniani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na serikali ya Uingereza inaeleza kuwa athari za kuwasili kwa idadi kubwa ya wahamiaji kutoka EU ni mojawapo ya mambo makubwa ambayo yalisababisha raia wa Uingereza kupiga kura kwa wingi kuunga mkono Uingereza kujitoa katika Umoja wa Ulaya mwaka 2016.

Serikali imehamasisha waajiri kuacha kutegemea wafanyakazi wa kulipwa mshahara wa chini kutoka Ulaya na kuwekeza zaidi katika kudumisha wafanyakazi na kuendelezа teknolojia.

Serikali ya Uingereza iliwahi kusema katika miaka iliyopita kwamba inataka kupunguza wahamiaji wanaoingia nchini humo.

Pamoja na mfumo huo mpya wa uhamiaji viza zitatolewa kwa wahamiaji kulingana na ujuzi wao, kiwango cha elimu, mshahara au taaluma. Wakati mchakato huo mhamiaji atakuwa anapewa alama 50 iwapo atatimiza vigezo hivyo.

Kwa ujumla itakuwa lazima kwa mhamiaji kufikisha alama 70 ili aweze kufanya kazi Uingereza huku pia akipata alama kulingana na kiwango chake cha elimu, mshahara atakao kuwa anapokea na kufanyakazi katika sekta zenye upungufu. **RFI**

# Idadi waliofariki na Corona yafikia 2,000

**BEIJING,** China

MAOFISA nchini China wamesema idadi ya watu waliofariki kutokana na ugonjwa wa virusi vya Corona imefikia 2,004, huku zaidi ya 74,000 wakiwa wameambukizwa.

Wakati idadi hiyo ikitolewa, nako mjini Hong Kong taarifa zinaeleza kuwa mtu wa pili aliyekuwa ameambukizwa amefariki dunia.

Mataifa mengine ambayo yameripoti vifo kutokana na virusi vya Corona ni pamoja na Ufaransa, Japan, Ufilipino na Taiwan.

**Nako Hong Kong taarifa zinaeleza kuwa mtu wa pili aliyekuwa ameambukizwa amefariki dunia.**

Wakati huohuo, abiria waliokuwa wamekwama katika meli iliyokuwa imetengwa kwa hofu ya kuwa na abiria walioambukizwa ugonjwa virusi hivyo unaofahamika kama Covid-19 na kuzuiliwa katika bandari ya Yokohama nchini Japan kwa muda wa siku 14 wameanza kuondoka ndani ya meli hiyo.

Baada ya kuondoka ndani ya meli hiyo abiria wamekuwa wakielezea namna ilivyokuwa ngumu kwao kusalia ndani ya meli hiyo kwa siku 14, baada ya kuripotiwa kuwa abiria 542 walikuwa wameambukizwa virusi hivyo.

Hatua ya kuwaruhusu abiria hao ilikuja baada ya kufanyiwa vipimo na kubainika kuwa walikuwa hawajaambukizwa, huku wale walioambukizwa wakiendelea kutengwa kwa muda zaidi kwa siku kadhaa kwa sababu za kiafya. **RFI**



Waziri wa mambo ya nje wa Marekani Mike Pompeo (kushoto) akiwa nchini Ethiopia katika moja ya ziara yake. **PICHA: REUTERS**

# Tweet za Rais Donald Trump zamkera Mwanasheria Mkuu, afikiria kujiuzulu

**WASHINGTON,** Marekani

IDADI ya washirika wa Rais Donald Trump inaendelea kupungua wakati Mwanasheria Mkuu, William Barr akifikiria kujiuzulu, sababu kuu ikiwa ni kuchukizwa na 'tweet' za Rais Trump dhidi ya idara ya mahakama.

Idara ya Mahakama nchini Marekani huenda ikapata pigo baada ya Barr kuripotiwa kuweleza watu wa karibu wa Rais Trump kuhusu wasiwasi wake juu ya Tweet za Trump.

Hata hivyo, haijabainika wazi iwapo mwanasheria huyo mkuu amemueleza Rais Trump moja kwa moja juu ya nia yake.

Taarifa zinaeleza kuwa Barr huenda amewaeleza watu wa karibu wa Rais Trump juu ya kadhia yake akiwa na lengo kuwa ujumbe wake utamfikia Trump ili aache kuandika hisia zake kwenye mitandao ya kijamii kuhusu uchunguzi wa idara ya mahakama.

Ikulu ya Marekani na Idara ya mahakama haijatoa tamko lolote kuhusu suala hilo la Mwanasheria Mkuu kutafakari kujiuzulu licha ya ombi la Gazeti la Washington Post kutaka maoni kutoka kwao.

Hata hivyo, Msemaji wa Idara ya Mahakama, Kerri Kupec alipuuzia mbali tetesi hizo za Barr kuwa na nia ya kujiuzulu na kuzitaja kama porojo tu.

Kupec aliandika kwenye mtandao wake wa Twitter kuwa: "Mwanasheria Mkuu hana mpango wa kujiuzulu".

Haya yanajiri baada ya Rais Trump kusema kuwa ana imani na utendaji kazi wa Barr, ambaye wiki iliyopita alisema katika mahojiano kuwa tabia ya Rais Trump ya kuandika kwenye mitandao ya kijamii ilikuwa inatatiza kazi yake.

Hata hivyo, Rais Trump naye alikiri mbele ya waandishi habari kuwa ni kweli anaifanya kazi ya Barr kuwa nguvu. Hata hivyo, alimsifu Mwanasheria Mkuu huyo kwa kumtaja kuwa ni mtu mwenye uadilifu mkubwa.

Licha ya Barr kukerwa na tabia ya Rais Trump ya kutumia mitandao ya kijamii, Rais huyo wa Marekani anaonekana kupuuza wito wa kumtaka akomeshe tabia hiyo kwa kusema anahisi mitandao ya kijamii ni muhimu kwani imempa nafasi ya kuwa na sauti.

Wiki iliyopita maofisa katika idara ya mahakama walimuondolea hukumu rafiki wa karibu wa RaisTrump, Roger Stone, aliyepatikana na hatia ya kulidanganya bunge la Congress Novemba, mwaka jana.

Rais Trump alitumia mtandao wa Twitter kuwashambulia waendesha mashtaka wanne pamoja na Jaji ambao walikuwa wanaiskiliza kesi ya Stone. **DW**

# Hukumu faini 300,000/- aliyeua mke yakosolewa

**Na Mwandishi Wetu**

HUKUMU iliyotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma ya kumtaka kulipa faini ya Sh. 300,000 aliyeshtakiwa kwa kosa la kuua bila kukusudia, imezua mjadala mzito huku baadhi ya wanasheria wakiipinga na kudai hakuna sheria ya namna hiyo.

Juzi, Nipashe ilichapisha habari ya mahakama hiyo kumhukumu kulipa faini ya Sh. 300,000 mkazi wa Kijiji cha Kiyungwe wilayani Kasulu kwa kosa la kumuua mke wake kwa kipigo Agosti 15, 2018.

Katika mtandao wa Twitter wa Nipashe, baadhi ya watu walihoji kuhusu hukumu hiyo iliyotolewa ambapo mfuasi wa akaunti hiyo anayetumia jina la Prisla Steve aliuliza: "Kwamba thamani ya uhai sasa hivi ni 300,000/-, kweli tunaangamia kwa kukosa maarifa.

Kutokana na watu wengi kuhoji kuhusu hukumu hiyo, Nipashe ilimtafuta Mwanasheria na Rais wa zamani wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume, kutoa ufafanuzi wa kisheria kuhusu hukumu hiyo.

Fatuma alidai Sheria ya Kanuni za Adhabu inatamka katika Kifungu Namba 198 kinachohusu makosa ya jinai kuwa ukiua bila kukusudia, adhabu yake yaweza kuwa kifungo cha maisha jela.

"Kwa hiyo, jaji anaweza kukufunga mfano miaka 10, miaka mitano au miwili, lakini siyo kukulipisha faini, hakuna faini ya kumtoa mtu roho, yaani mume amemtoa mke wake roho, Mahakama Kuu ya Kanda inamlipisha mume faini ya Sh. 300,000/-.

"Ukikubali faini kwa kutoa roho ya mtu ni kuruhusu matendo ya mauaji kwenye jamii kuendelea kutendeka, yaani mtu anaua akijua mahakama itamlipisha faini 300,000, huwezi kuweka bei kwenye roho ya binadamu, hii siyo sheria," alidai.

Akisoma maelezo ya kesi hiyo, Wakili wa Serikali, Happy Mayunga, alidai mshtakiwa Msafiri Ntarakila (68), alitenda kosa hilo usiku baada ya kurudi nyumba kwake akiwa amekunywa pombe na kutomkuta mke wake nyumbani.

Mayunga alidai mshtakiwa baada ya kumkosa mke wake alimtafuta na kumpata ndipo alipoanza kumpiga sehemu mbalimbali za mwili, hatua iliyosababisha mwanamke huyo kuvuja damu nyingi kutokana na majeraha.

Alidai kuwa watu walioishi karibu, walisikia kelele na kwenda kutoa msaada wa kumpeleka hospitali mwanamke huyo ambaye hata hivyo alipoteza uhai akiwa njiani.

Awali, Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ivin Mugeta, aliyesikiliza kesi hiyo, alimhoji mshtakiwa kama alitenda kosa hilo na mshtakiwa alikiri kutekeleza mauaji dhidi ya mke wake.




Meneja Masoko wa Benki ya NBC, Alina Maria Kimaryo (kulia), akikabidhi zawadi ya bodaboda kwa Rosemary Kibodya, baada ya kuibuka mshindi katika droo ya Mwezi Desemba ya Kampeni inayoendelea ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo ya benki hiyo. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana pamoja na droo ya mwezi Januari, ambapo washindi watano walijishindia bodaboda moja mpya kila mmoja. Kushoto ni Meneja Tawi la NBC Corporate, Mariam Kombo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Awataka wachimbaji madini kupanda miti

**Na Robert Hokororo,** IRAMBA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amewataka wachimbaji wadogo kuhifadhi mazingira katika maeneo yao ya machimbo kwa kupanda miti.

Sima alitoa agizo hilo jana akiwa katika ziara yake ya kutembelea wachimbaji wa machimbo ya Sekenke 1 wilayani Iramba mkoani Singida.

Katika ziara hiyo ya kuangalia namna wachimbaji wanavyotunza mazingira pamoja na kuwapa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya kemikali ya zebaki, Sima alisema ni wajibu kwao kuhakikisha hawakati miti ovyo ili kulinda mazingira.

Alisema serikali inatambua mchango wa wachimbaji wadogo nchini na ndiyo maana imeridhia Mkataba wa Minamata kuhusu matumizi ya zebaki na kuwa pamoja na hatua hiyo, inasisitiza upandaji miti na kutunza mazingira.

Alisema ni jukumu la serikali kuhakikisha uchimbaji wa madini unakuwa salama kwa mazingira.

"Maisha yetu yanategemea mazingira safi na salama, lakini wakati tunaendelea kutembea katika eneo hili, tumeona miti ni michache, kiafya hii si salama.

"Niwaombe mwakilishi wa Mkurugenzi, mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na watu wa madini, eneo hili lipandwe miti ya kutosha ili tutunze mazingira," aliagiza.

Naibu Waziri huyo pia aliwataka wachimbaji hao kutafuta mbadala wa matumizi ya miti ambayo wanakata kwa ajili ya kuimarisha kuta za mashimo wakati wanafanya shughuli za uchimbaji.

Sima alisema Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki ulioridhiwa na Tanzania hivi karibuni, una kipengele kinachosisitiza uanzishwaji wa vikundi vya wachimbaji.

Alisema hatua ya kuanzisha vikundi itarahisisha ukopeshaji kwa urahisi kupitia taasisi za fedha zikiwamo benki nchini kuliko ambavyo inavyokuwa kwa mmoja mmoja.

Ofisa Mazingira Mkoa wa Singida, Charles Kidua, alisema takriban hekta 400,000 za misitu hupotea kila mwaka kutokana na ukataji wa miti.

Kidua alisema ili kuepusha nchi kugeuka jangwa, serikali imekuwa ikiendelea kuwataka wananchi wapande miti kwa wingi na kupunguza kuikata.

# Sekta ya fedha kuimarishwa

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesema itaifanyia kazi sekta ya fedha kwa kuimarisha sera ili iweze kuchangia kiasi kikubwa katika pato la Taifa.

Imesema kwa kufanya hivyo, itakuwa tofauti na hali ilivyo sasa, ambapo mchango wa Sekta ya Fedha ni asilimia 4.1 pekee .

Akizungumza katika uzinduzi wa mauzo ya hisa ya Yetu Benki jijini Dar es Salaam juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, alisema kunachangamoto za kimfumo katika sekta hiyo, ambazo zimekuwa zikizorotesha jitihada zinazofanyika katika kuiboresha sekta ya fedha, inayochangia masharti ya mikopo kutokuwa nafuu.

"Nafahamu fika kuwa baadhi ya changamoto nyingi ni za kimfumo, kwa mfano ukosefu wa uwekezaji wa mitaji ya muda mrefu ambayo ingeweza kuleta unafuu katika utoaji mikopo katika benki zetu," alisema Kairuki.

Aidha, alisema kuna changamoto zingine za kimtazamo na kimuundo ambazo alisema zinaweza kutatuliwa kwa ushirikiano wa mamlaka za Serikali ikiwamo Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ,mamlaka ya masoko ya dhamana na mitaji, Soko la Hisa la Dar es Salaam, Mfuko wa kuendeleza Sekta ya Fedha pamoja na wawekezaji mbalimbali wa sekta hiyo.

Alieleza kuwa kuanzishwa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam ni kwa lengo la kuziwezesha kampuni kuongeza mitaji kwa kuuza hisa zake kwa wananchi, na kuwataka wawekezaji kutafuta njia mbadala zaidi ya ile ya kuuza hisa kwa kubuni sera na mikakati mbalimbali kuliko kuiga zile zizoeleka katika nchi zilizoendelea .

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki Yetu , Altemius Milinga, alisema benki hiyo ni ya wananchi kwa vile imeanzishwa na raia wa Tanzania na ina lenga katika kuwainua wananchi wa kawaida ikiwamo wanaofanya biashara za mitaji midogo .

"Mheshimiwa Waziri, Benki hii imeanzishwa na Watanzania na ndio wenye hisa nyingi, na wateja wetu ni wananchi wote wakiwamo wenye mitaji midogo midogo," alisema Milinga.

**Mheshimiwa Waziri, Benki hii imeanzishwa na Watanzania na ndio wenye hisa nyingi, na wateja wetu ni wananchi wote wakiwamo wenye mitaji midogo midogo.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. MWENYE NYUMBA **0757 804 970**



***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


**KUPOTEA KWA CHETI**



**PASCHAL HERMAN DUDIYECK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2913/0081** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MANG'OLA SEKONDARI mwaka 2015.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/204813/2019.**

115637802

**KUPOTEA KWA CHETI**



**OMARI RAMADHANI MAKARAMANGI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S0321-0354 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KINONDONI SEKONDARI, November 1995.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/153564/2020.

115637402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;33/2020**

Ombi la ASHA BAKARI RASHID Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANIFA BAKARI RASHID

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 27/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/02/2020.

215637702

**WIZI WA GARI**

ZUBERI CHILILO MSISI anatangaza kupotelewa na gari aina ya TOYOTA IST yenye namba za usajili T 595 DSQ. Chassis No.NCP605000863, Engine No.2NZ4249164, ya mwaka 2006. Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/144882/2020.

115637602


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# CASILLAS KUSTAAFU AWANIE URAIS RFEF




**LISBON,** Ureno

GWIJI wa Hispania, Real Madrid na Porto, Iker Casillas anapanga kustaafu soka baada ya kutangaza kuwania urais wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), kwa mujibu wa rais wa Klabu ya Porto, Jorge Nuno Pinto da Costa.

Casillas alikumbwa na shambulio la moyo wakati akiwa kwenye mazoezi na klabu ya Porto Mei mwaka jana, ingawa hajacheza tangu kipindi hicho, golikipa huyo mwenye umri wa miaka 38, hakutangaza kustaafu soka licha ya kuongezwa kwenye benchi la timu hiyo Julai.

Alijumuishwa kwenye kikosi cha Porto kwa ajili ya msimu wa 2019-20, lakini tangazo lake la Jumatatu la kuwania uongozi wa Shirikisho la Soka la Hispania inamaanisha kwamba atathibitisha kustaafu kwake haraka.

Ingawa kipa huyo hajazungumza hadharani kuhusu jambo hilo, Pinto da Costa amedai kwamba Casillas alimuambia siku zake za kucheza zimefikia mwisho, wakati akiwania kuchukua mikoba ya Rais wa RFEF, Luis Rubiales.

"Nina furaha kubwa. Casillas ana mtazamo ambao umenigusa mimi, kwa sababu kabla ya kutangaza mpango wa kugombea alikuja Porto na kubainisha kwamba angependa kuchukua maamuzi ya kustaafu kucheza soka," alisema Pinto da Costa akiwaambia waandishi wa habari Jumanne.

"Amekuwa na wakati mzuri, kwani amecheza kwenye klabu mbili tu na tunajua kwamba ana mapenzi na timu zote mbili."

Casillas alicheza jumla ya mechi 167 kwa kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania na alikuwa nahodha wa timu yake kwenye fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2010 pamoja na michuano ya Ulaya mwaka 2008 na 2012.

# Klopp asema atawanyoosha Atletico Anfield

**MADRID,** Hispania

JURGEN Klopp ameionya Atletico Madrid kwamba, Anfield itakuwa sehemu ya mapigano makali kama ilivyotokea kule kwenye dimba la Wanda Metropolitano wakati Liverpool ikiangalia uwezekano wa kupindua matokeo baada ya kupoteza kwa bao 1-0 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

Bao la Saul Niguez la dakika ya nne lilitosha kuwapa ushindi miamba hao wa Hispania mbele ya mabingwa hao watetezi.

Uwanja wa Madrid ulikuwa mgumu kwa Liverpool Jumanne wakati kocha wa Atletico, Diego Simeone alipoonekana kuwahamasisha vilivyo mashabiki wake.

"Mashabiki wa Atletico ambao wanaweza kupata tiketi nawakaribisha Anfield," alisema Klopp.

"Hisia ni muhimu. Usiku ule kwa vyovyote ulikuwa mzuri zaidi kwa Atletico, lakini naangalia mbele kuelekea mchezo wa pili.

"Tunazungumza kuhusu muda na nguvu ya Anfield na hasa ukiangalia nguvu iliyokuwapo Anfield.

"Hadi mapumziko tulikuwa nyuma kwa bao 1-0. Mchezo wa pili utachezwa kwenye uwanja wetu na tutakuwa na hisia nzuri."






# *Emre Can sasa jumla Dortmund*

**DORTMUND,** Ujerumani

EMRE Can atajiunga na Borussia Dortmund kwa mkataba wa kudumu kutoka Juventus Julai mwakani kwa dili litakalomuweka hapo hadi mwaka 2024, klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, imetangaza.

Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 26, awali alihamia Dortmund Januari kwa mkopo ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Alifunga bao lake la kwanza kwenye mchezo wake wa kwanza kucheza Bundesliga wakati wakipoteza 4-3 kwa Bayer Leverkusen na alianza wiki iliyopita wakati wakiifumua 4-0, Eintracht Frankfurt.

Awali kulikuwa na kipengele kwenye mkataba huo wa mkopo kwamba Dortmund watamnunua mchezaji huyo kwa euro milioni 25 kama kiwango chake kitaimarika na sasa klabu hiyo imekubali kumchukua ikiwa ni siku 18 tangu ahamie hapo.

"Klabu ya Bundesliga, Borussia Dortmund imefikia makubaliano na mabingwa wa Italia, Juventus juu ya kumnunua kwa mkataba wa kudumu mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani Emre Can," ilisomeka taarifa ya Dortmund kwenye tovuti yake.

"Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, mkataba wake wa mkopo ulikuwa unamalizika Juni. Hivyo kuanzia Julai Mosi atakuwa na mkataba mpya na Borussia Dortmund na Can atakuwa kwenye kikosi hiki hadi Juni 30, mwaka 2024."

Kiungo huyo wa zamani wa Bayern Munich na Leverkusen amerudi kucheza nchini Ujerumani kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka sita.

## HABARI MICHEZO



# NEYMAR AISHUTUMU PSG KUTORUDI UWANJANI

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Neymar ameishutumu klabu yake namna ilivyomchelewesha kurudi uwanjani baada ya kuumia mbavu na amesema alitakiwa kuchezeshwa haraka ili kuimarisha afya yake.

Baada ya kukosa mechi nne, Neymar alirudi uwanjani Jumanne na kuifungia PSG bao moja, wakati wakipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Borussia Dortmund kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

Neymar aliumia mbavu kwenye mchezo dhidi ya Montpellier Februari mwaka huu na nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa shakani kucheza dhidi ya Dortmund kabla ya kurudi katika kikosi hicho cha kocha Thomas Tuchel.

Hata hivyo, Neymar - ambaye aliisawazishia PSG dakika ya 75 kabla ya Erling Haaland kuifungia la pili Dortmund - hakuwa na furaha wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Ilikuwa ngumu baada ya kutocheza mechi nne. Haukuwa uamuzi wangu kucheza, klabu ilichukua uamuzi," alisema Neymar akiwaambia waandishi wa habari huku kukiwa na uvumi wa kutakiwa kurudi tena kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona.

"Klabu ilifanya uamuzi na timu ya madaktari. Nilitaka kucheza, nilijihisi vizuri."

## Son kukaa nje msimu mzima - Mourinho



**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amesema anatarajia mshambuliaji wake, Son Heung-Min kuukosa msimu mzima, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini akifanyiwa upasuaji baada ya kuvunjika mkono, klabu hiyo imetangaza.

Habari hizo zimekuja kama pigo kwa Spurs, ambao tayari wanamkosa mshambuliaji, Harry Kane hadi Aprili mwaka huu.

Na Tottenham awali ilimtarajia Son kuwa nje ya uwanja kwa wiki kadhaa," alisema Mourinho.

"Sitamhesabia tena msimu huu," alisema akiwaambia waandishi wa habari kuelekea kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora dhidi ya RB Leipzig.

Mourinho pia alisema kukosekana kwa Son kwenye mchezo huo kutamlazimu kubadilisha mfumo.

## *Kocha amvulia kofia Haaland*

**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA wa Borussia Dortmund, Lucien Favre, amemsifia Erling Haaland baada ya kuonyesha kiwango kilichoweka rekodi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Haaland aliweka historia kwa kufunga mabao mawili wakati Dortmund ikiifunga Paris Saint-Germain 2-1 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora juzi Jumanne.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amekuwa mchezaji aliyefunga kwa haraka zaidi mabao 10 kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akifikisha mabao hayo katika mechi saba tu alizocheza.

Haaland aliweka rekodi hiyo akichezea kwa mara ya kwanza Dortmund kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Favre alimsifia mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway, ambaye alitua hapo akitokea Salzburg Januari.

"Alicheza vizuri dhidi ya mwenzake," alisema Favre akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Pia alisimama vizuri na kuonyesha kiwango chake cha kuvutia zaidi pamoja na wachezaji wenzake. Ilitusaidia na alicheza kwa ushirikiano mzuri."

Rekodi nyingine alizoziweka Haaland - akiwa na umri wa miaka 19 na siku 212 - ni mchezaji wa kwanza mwenye umri mdogo kufikisha mabao 10 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu mmoja nyuma ya nyota wa PSG, Kylian Mbappe (ambaye alifikisha mabao hayo akiwa na umri wa miaka 18 na siku 360).



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK: ATLETICO MJUE BADO DAKIKA 90 ANFIELD

## Walishangilia kama wameshashinda jumla baada ya mechi, watakuja Anfield na tunajua…

**MADRID,** Hispania

VIRGIL van Dijk amekipotezea kipigo cha bao 1-0 Liverpool ilichokipata kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atletico Madrid akieleza kama bahati mbaya na kisha akaionya klabu hiyo ya Hispania kuwa bado kuna dakika nyingine 90 za mwisho kukamilisha hatua hiyo ya 16-bora.

**Bao la mapema kupitia kwa Saul Niguez juzi, Jumanne liliiweka mbele Atletico na kuwafanya mabingwa hao watetezi, Liverpool kusubiri mchezo wa marudiano katika Uwanja wa Anfield hapo Machi 11, mwaka huu.**

Saul aliuzamisha mpira kimyani baada ya mpira wa kona kuangukia katika njia zake na kikosi hicho cha Diego Simeone, Atletico kikaweza kutumia faida hiyo kwa kuulinda ushindi huo hadi mwisho.

Mabingwa watetezi hao wa Ulaya, Liverpool walimiliki mpira katika mechi hiyo iliyopigwa jijini Madrid, lakini wakashindwa kupiga shuti hata moja lililolenga goli, huku Mohamed Salah na Jordan Henderson wakipoteza nafasi zao nzuri za kufunga.

Licha ya kufungwa wakiwa Uwanja wa Wanda Metropolitano, hata hivyo, beki Van Dijk bado anaamini watafanya vizuri mechi ya marudiano zaidi ya wiki tatu zijazo.

"Tuliruhusu bao kutokana na mpira wa kona, nafasi ya kwanza kwao, na wala si kwa kutengeneza nafasi. Bahati kidogo," aliiambia BT Sport.

"Ujumbe wakati wa mapumziko ulikuwa kuendelea kucheza. Tulikuwa na mpira kwa asilimia kubwa ya mchezo, lakini kwa bahati mbaya hatukutengeneza nafasi nyingi. Bado tuna dakika nyingine 90 za kuweka mambo sawa.

"Ni namna wanavyocheza. Ni kidogo ya soka la Hispania pia na inabidi uzoee na tulilijua hilo na nahisi tulishughulikia vema pia."

Kwa kuzingatia maoni ya mchezaji mwenza, Andy Robertson aliyeshuhudia kelele nyingi za kushereheka jukwaani kwa muda wote kwake bado rekodi ya Liverpool nyumbani ni ya kuvutia.

"Tulionyesha kiwango kizuri na tunajua tunaweza kuwa bora. Tunayo mechi ya marudiano ya kuweka mambo sawa," Robertson alisema.

"Walishangilia kama wameshashinda jumla baada ya mechi. Watakuja Anfield na tunajua mashabiki wetu watakuwapo pale. "Tuliwapa mwanzo bora na mashabiki kupata kuwa nyuma yao kisha wanaanza kuanguka juu na kuingia chini ya ngozi kidogo."

## ZISIKUPITE

### POGBA AWEKWA SOKONI

KIUNGO Mfaransa Paul Pogba anatarajia kuondoka Manchester United majira haya ya joto, lakini klabu inahitaji zaidi ya pauni milioni 150 ili kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa sasa. ***(ESPN)***

### UPAMECANO AITAJA ARSENAL

BEKI wa RB Leipzig, Mfaransa Dayot Upamecano, 21, amesema anajua "siri", ya Barcelona na Arsenal kuwa miongoni mwa klabu zinazovutiwa naye. ***(RMC Sport, via Goal)***

### ATAKIWA KUMRITHI SANE

MANCHESTER City inamtaka mshambuliaji wa Bayern Munich, Serge Gnabry, 24, kama sehemu ya mpango wa miamba hiyo ya Ujerumani kumrejesha Bundesliga winga wao Mjerumani Leroy Sane, 24. ***(Sun)***

### LAMPARD HALI TETE CHELSEA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, atakuwa katika uchunguzi mkubwa kama klabu hiyo itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. ***(Telegraph)***

### UEFA KUICHUNGUZA ZAIDI CITY

MANCHESTER City inaweza kukabiliwa na uchunguzi zaidi kutoka Uefa katika kiwango cha udhamini wa Abu Dhabi walichotangaza baada ya kufungiwa kushiriki michuano ya Ulaya kwa kuvunja sheria ya manunizi ya wachezaji kulingana na pato la klabu, FFP. ***(Guardian)***

### GIROUD ASUBIRIWA LAZIO

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, 33, amepewa ofa ya kujiunga na Lazio wakati mkataba wake utakapomalizika majira ya joto. ***(Le10 Sport, via Star)***

### SAKA KUPEWA MI5 ARSENAL

ARSENAL inataka kumsainisha winga wao, Bukayo Saka, 18, mkataba mpya wa miaka mitano kufuatia huu wa sasa kubakiza miezi 18 kabla ya kumalizika, wakati huu Liverpool, Manchester United na Bayern Munich zote zikivutiwa na nyota huyo wa kimataifa wa England U-19. ***(Mirror)***

### HENRIQUE AMULIKWA UNITED

MANCHESTER United inazingatia uwezekano wa kumnasa Mkurugenzi wa Soka wa zamani wa Paris St-Germain, Antero Henrique na Mkuu wa Idara ya Michezo wa Red Bull, Ralf Rangnick ikitaka kuwapa kazi ya Ukurugenzi wa Ufundi. ***(Independent)***

### BELLINGHAM AVUTA VIGOGO

CHELSEA inamfuatilia kiungo kinda wa Birmingham City, Jude Bellingham, 16, lakini Manchester United, Barcelona na Real Madrid pia zimekuwa zikihusishwa na nyota huyo wa kimataifa wa England U-17. ***(Goal)***

### YAMGEUKIA BRAITHWAITE

BARCELONA imemgeukia mshambuliaji wa Laganes na Denmark, Martin Braithwaite, 28, kama windo lao kuu baada ya kuruhusiwa kusajili mbadala wa majeruhi Mfaransa Ousmane Dembele, 22, na imeweka kando kuvutiwa kwake na straika wa Real Sociedad, Mbrazil Willian Jose, 28. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Tshishimbi awatoa hofu mashabiki

**Na Saada Akida**

WAKATI huu wakiwa katika vita vya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara, nyota Yanga wameweka mikakati ya kuhakikisha wanaongeza umakini ili kutimiza majukumu yao ndani ya uwanja na kufikia malengo yao ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi, jana aliliambia Nipashe kuwa wana kila sababu ya kushinda katika michezo ya ligi na Kombe Shirikisho la Azam (FA Cup) kwa ajili ya kutafuta nafasi ya kucheza kimataifa.

Alisema hawajakata tamaa na matokeo ya michezo yao iliyopita na kwamba wana imani ligi bado ndefu, hivyo watapambana katika mechi zao hizo pamoja na Kombe la FA ambalo ni muhimu kushinda katika michuano hiyo itakayowapa nafasi ya kufikia kile kinachotarajiwa kukifikia na Wanayanga.

"Kwa sasa tunaangalia mbele kwa mbele, hatuna sababu ya kurudi nyuma, tulikotoka hatukuwa katika hali nzuri, ila kwa sasa timu ipo vizuri, wachezaji wote tuna morali ya juu," alisema nahodha huyo.

Yanga iliyopo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 40, itashuka tena dimbani Jumapili kuvaana na Costal Union katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga baada ya juzi kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania mjini Moshi.

## Mgunda aipigia hesabu Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukubali kipigo cha mabao 2-1 nyumbani dhidi ya Ruvu Shooting, Kocha Mkuu wa timu ya Coastal Union, Juma Mgunda ameanza kuchukua tahadhari kuelekea mechi ijayo watakapoikaribisha Yanga katika Uwanja wa Mkwakwani.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda alisema, jana aliwapumzisha wachezaji wake kufanya mazoezi ya asubuhi kabla ya kuendelea na programu hiyo jioni, kutokana na uchofu wa mchezo uliopita dhidi ya Ruvu Shooting.

"Leo (jana) nimewapumzisha wachezaji wangu kufanya mazoezi ya asubuhi mpaka jioni ili kupunguza uchovu walionao baada ya kumaliza mchezo wetu wa juzi na timu ya Ruvu Shooting ," alisema Mgunda huku akiahidi kufanyia kazi makosa aliyoyabaini katika michezo iliyopita.

Alisema walipoteza mchezo uliopita kutokana na wachezaji wake kufanya makosa madogo madogo ambayo yaliwagharimu katika kuvuna pointi tatu licha ya kuwa wenyeji wa mchezo huo.

Alisema watapambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wao wa Jumapili dhidi ya Yanga licha ya kwamba ni wazi utakuwa na ushindani mkubwa.

# HAMSINI ALIA POLISI KUDHULUMIWA BAO

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU akilalamika "kudhulumiwa" bao lao la wazi kabisa, Kocha Mkuu wa timu ya Polisi Tanzania, Malale Hamsini ameeleza kufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake juzi walipokutana na timu ya Yanga kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi na kutoka sare ya bao 1-1.

**Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kutoka mkoani Kilimanjaro, Malale alisema licha ya Yanga kuwa timu kubwa, vijana wake walipambana na kupata mabao mawili ingawa moja lilikataliwa na mwamuzi.**

"Nashukuru tumepata pointi moja nyumbani japo tumedhulumiwa goli letu kama si hivyo, naamini jana tungepata pointi tatu nyumbani, tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono,"alisema Malale.

Kuhusu maandalizi ya mechi yao ijayo nyumbani Jumamosi dhidi ya Ruvu Shooting, Malale alisema aliendelea kukinoa kikosi chake kwa ajili ya kuhakikisha anavuna alama tatu.

"Leo tumeendelea na mazoezi kama kawaida kwa ajili ya kuwaweka fiti wachezaji wangu kujiandaa na michezo mingine ijayo, lengo ni kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu ," alisema.

Aidha, alisema mapungufu aliyoyabaini katika mchezo uliopita anaendelea kuyafanyia kazi ili yasiweze kujitokeza kwa mara nyingine ikiwa ni pamoja na kuwataka wachezaji wake kuzidi kuongeza juhudi pindi wawapo dimbani.

Alisema suala la waamuzi kutokufuata sheria za mpira bado limeendelea kuwa sugu kutokana na kutoridhishwa na maamuzi yaliyofanywa na mwamuzi aliyechezesha mchezo kati yao na mahasimu wao Yanga.

Katika mechi hiyo ya juzi, Yanga ilikuwa ya kwanza kupata bao la kuongoza kupitia kwa Tariq Seif dakika ya 40, hata hivyo Polisi Tanzania wakasawazisha bao hilo dakika ya 67 likifungwa na mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Matheo Anthony kwa kichwa akimalizia krosi ya Sixtus Sabilo, ambalo hata hivyo lilikataliwa.

Refa Abel William alimfuata msaidizi wake namba moja, Martin Mwaliaje kushauriana naye na wakalikataa bao hilo.

Lakini Polisi Tanzania hawakukata tamaa na kwa kutumia makosa ya aina ile ile ya safu ya ulinzi ya Yanga, wakafanikiwa kupata bao lingine dakika tatu baadaye, mfungaji akiwa Sabilo akimalizia pasi ya Marcel Kaheza dakika ya 71.




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), akishangilia sambamba na straika mwenzake, John Bocco, baada ya kuifungia timu yake bao pekee kwa penalti wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Taifa juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Shime asifu kiwango Twiga Stars*

**Na Somoe Ng'itu,** TUNISIA

LICHA ya timu yake kupoteza mchezo dhidi ya Morocco, Kocha Mkuu wa timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesifia kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo huo.

Twiga Stars, ambayo ni timu alikwa, ilifungwa mabao 3-2 dhidi ya Morocco juzi, lakini imeendelea kukaa kileleni katika msimamo wa mashindano hayo yanayoshirikisha nchi tano za Ukanda wa Afrika Kaskazini.

Akizungumza na Nipashe nchini hapa, Shime alisema wachezaji wake wamepata somo kubwa katika mechi hiyo na kila mchezaji alifuata malekezo aliyotoa katika mechi hiyo.

Shime alisema anahitaji kuona kiwango kilichoonyeshwa katika mechi hiyo kinaendelezwa katika mchezo wa mwisho dhidi ya wenyeji, Tunisia utakaochezwa Jumamosi.

Kocha huyo alisema licha ya mchezaji wake mmoja kuonyeshwa kadi nyekundu juzi, kikosi chake kiliendelea kucheza kwa kiwango cha juu na hatimaye kilifanikiwa kupata bao na kumiliki mpira kwa kiwango kikubwa.

"Nawapongeza sana wachezaji wangu, walicheza katika kiwango cha juu, walifuata maelekezo vizuri na walitekeleza maagizo kwa asilimia kubwa, tumejifunza na tumepata somo zuri kupitia mechi ile (dhidi ya Morocco)," alisema Shime.

Naye Mwanahamisi Omary "Gaucho" alisema anafurahi kuwa sehemu ya kikosi cha Twiga Stars kinachoshiriki michuano hii na anaamini ataendelea kujituma atakapopata nafasi katika mchezo wa mwisho.

"Haya matunda tunayoyaonyesha ni jitihada na mipango ya TFF katika kuendeleza soka la wanawake, tunaahidi tutaendelea kupeperusha vema bendera ya nchi katika kila mashindano tutakayoshiriki," alisema Gaucho.

Mashindano hayo yanatarajiwa kuendelea tena leo kwa wenyeji Tunisia kucheza dhidi Algeria wakati Morocco wakiwakaribisha Mauritania huku Twiga Stars ikipumzika.

# Michezo

Alhamisi Februari 20, 2020

Nipashe




Van Dijk: Atletico mjue bado dakika 90 Anfield UKURASA 30

MTU KATI...




Mabeki wa Atletico Madrid wakimweka mtu kati mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, katika mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano na Atletico kushinda 1-0 juzi. **HABARI UK. 28**

## Maxime: Simba hii tungepigwa nyingi

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, akieleza kufurahishwa zaidi na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake na wala hatazami ushindi kiduchi walioupata, Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema kikosi chake kilistahili kupigwa mabao mengi zaidi.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi usiku, Simba ilishinda kwa bao 1-0, shukrani kwa Meddie Kagere aliyefunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 60 baada ya Jonh Bocco kuchezewa madhambi ndani ya 18 na kipa Benedict Tinoco.

Akizungumzia mchezo huo, Maxime alisema wachezaji wake hawakucheza vizuri na kuwaruhusu Simba kumiliki mpira, jambo ambalo liliwafanya wapinzani wao hao kucheza kwa kiwango bora na kwamba kama Wekundu wa Msimbazi hao wangekuwa makini, wangewafunga idadi kubwa zaidi ya mabao.

"Si busara kukaa mbele za watu kuwalaumu wachezaji, kikubwa hatukucheza vizuri, ninawajua wachezaji wangu tulishindwa kumiliki mpira na kuwapa nafasi Simba kuweza kutushambulia,"alisema.

Kwa upande wa Sven, alisema amerìdhishwa zaidi na kiwango kizuri cha soka kilichoonyeshwa na wachezaji wake dhidi ya Kagera Sugar na anahitaji kuona wanaendelea kujituma na kujitolea kwa kiwango bora kama hicho katika kila mchezo.

"Kiwango hiki walichokionyesha leo (juzi), ndio nahitaji kukiona katika michezo ijayo, huu ndio mpira ambao Simba wanacheza, sijali idadi ya bao 1-0 tuliloshinda, ni ndogo ila nimeridhishwa zaidi na kile kilichofanywa na vijana wangu," alisema.

# Yanga: Ubingwa njia nyembamba

## ●●● Kocha akiri wana kazi ya kufanya kuishika Simba huku wakiipania Coastal Union kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutoka sare ya tatu mfululizo kwa kunusurika kipigo dhidi ya Polisi Tanzania, Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface Mkwasa, amesema wamezidi kuifanya njia ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kuwa nyembamba zaidi.

**Ikiwa katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi juzi, licha ya Yanga kutangulia kupata bao la kuongoza kupitia Tariq Seif dakika ya 40, ilijikuta dakika 90 zikimalizika kwa sare ya bao 1-1 huku Polisi Tanzania wakimlalamikia mwamuzi Abel William na msaidizi wake namba moja, Martin Mwaliaje kwa kuwanyima bao la wazi.**

Ushindi wa mwisho kwa Yanga ulikuwa Februari 8, mwaka huu, ilipoichapa Ruvu Shooting bao 1-0, lakini baada ya hapo ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City, kabla ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Tanzania Prisons, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia mechi hiyo ya juzi, Mkwasa kwa maoni yake aliwasifu waamuzi kwa kuchezesha kwa haki lakini akieleza wamezidi kuifanya njia ya kutwaa ubingwa kuwa nyembamba, wakati huu watani zao Simba wakiwa kileleni na alama 59 baada ya kushuka dimbani mara 23.

"Tumezidi kuifanya njia ya ubingwa kuwa nyembamba, ila tutaendelea kupambana kwa kuwa ligi bado ni ndefu na sasa tunajipanga kwa ajili ya mechi ijayo [dhidi ya Coastal Union] Jumapili.

"Kuhusu waamuzi walikuwa 'fea' wanapofanya vizuri lazima tuwapongeze, makosa mengine ni ya kibinadamu," alisema Mkwasa, ambaye matokeo hayo yanawafanya kufikisha pointi 40 sawa na Namungo FC iliyoishusha hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, lakini Yanga ikiwa nyuma kwa michezo miwili.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alilalamikia timu yake kudhulumiwa bao lao la dakika ya 67 kupitia kwa Matheo Anthony lililokuwa la kusawazisha, lakini refa Abel William aliimfuata msaidizi wake namba moja, Martin Mwaliaje na kushauriana kabla ya kulikataa.

Bao hilo lilifungwa kufuatia Matheo kuitendea haki krosi ya Sixtus Sabilo kwa kuiunganisha nyavuni kwa kichwa, lakini licha ya kukataliwa, dakika ya 71 Sabilo alifanya kweli kwa kuizamisha nyavuni krosi ya Marcel Kaheza na kufanya matokeo kuwa 1-1.

Hamisi alisema mwamuzi hakuwatendea haki kwa kulikataa bao hilo la wazi, lakini hawana budi kuheshimu uamuzi wake na kwamba hataki kuongea sana kuhusu hilo ili kuepuka kufungiwa.

"Nikiongea mengi nitawaudhi watu nitafungiwa, mimi lile ni bao la wazi, sijui kwa nini mwamuzi alilikataa," alisema Malale.

Yanga tayari imetua jijini Tanga tangu jana kwa ajili ya mechi yao ya Jumapili dhidi ya Coastal Union wakati Polisi Tanzania wakibaki nyumbani kuikaribisha Ruvu Shooting waliotoka kuwanyoa 'Wagosi wa Kaya' hao kwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Mkwakwani juzi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >